Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 72 No. 165 | SHA'BAN 1432 AH | JULAI 2011 | WAFA 1390 HS | BEI TSH. 500

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga Saumu kama walivyolazimishwa wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu.

Kwa siku zilizohesabiwa. Lakini miongoni mwenu awaye mgonjwa au katika safari, basi atimize hesabu katika siku zingine. Na wale wanaoweza, watoe fidia kwa kumlisha maskini. Na atakayefanya wema kwa radhi ya nafsi yake, basi ni bora kwake; na kama mkifunga ni bora kwenu, ikiwa mnajua. (*Al-Baqara, 2:184-185*).

Masih Aliyeahidiwa a.s. ajibu swali:

Nini hasa maana ya Jihad?

Dhana ya Jihad na maana yake hasa ni ngumu kueleweka kiasi ya kwamba watu wa zamani na wa leo wameshindwa kumaizi maana ya dhati ya dhana hii na hivyo kufanya makosa makubwa. Lazima tukiri ya kwamba makosa hayo yametoa mwanya kwa maadui wa Islam waweze kuikejeli na kuibeza dini hii tukufu. Dini ambayo ni dhihirisho la maumbile na inadhihirisha utukufu wa sheria za Mwenyezi Mungu.

Ni lazima ikumbukwe kuwa mzizi wa neno Jihad ni Juhud - ambalo maana yake ni kufanya juhudi, kufanya bidii. Pia limetumika kwa lugha ya majaaz ikiwa na maana ya vita vya kidini. Miongoni mwa Wahindi jina kwa ajili ya mapambano ya vita ni Yudah. Inaonyesha ya kuwa neno hili pia linatokana na neno Jihad. Kiarabu ni mama ya lugha zote. Na kila lugha chimbuko lake ni Kiarabu. Neno Yudah katika lugha ya Sanskrit maana yake ni mapambano, vita ambavyo vinatokana na neno Jihad au Juhud.

Sasa ningependa kuzungumza juu ya Jihad ni nini, na kwa nini Islam ilihitaji Jihad. Hivyo ni vyema kukumbuka kuwa Isalm ilipambana na misukosuko toka kuzaliwa kwake. Mataifa yote yalisimama kidete kupambana na kutaka kung'oa mzizi wa Islam. Kila anapodhihiri Mtume wa Mwenyezi Mungu na wafuasi wake wakionekana wacha Mungu wenye nia thabiti na wenye kutaka kwenda mbele ni dhahiri kuwa roho zenye husuda na wivu hutokota kwa hasira. Kudhihiri kwa Nabii wa Mwenyezi Mungu huwaondolea heshima waliokuwa na heshima na pato kwa waliokuwa na pato. Wapendwa wao huwaacha kwani wanakuwa wameonja utamu wa imani. Taqwa, elimu ya kimbinguni kutoka kwa Nabii wa Mwenyezi Mungu. Hivyo wale walionekana wenye busara na wenye maana huona kwamba busara si mali yao tena. Majina yenye heshima na makubwa yote hudidimia. Nyota ya waaminio hung'ara, kiongozi huyo mpya huheshimiwa na wale wengine waliokuwa na heshima hubaki wakisononeka na kutawaliwa na wivu hivyo hufanya kila jitihada za kuwapinga walopata nuru kutoka mbinguni. Kufika kwa manabii wa Mwenyezi Mungu huweka bayana nuru na hulitenga mbali giza na watu huanza kuvutwa kwenye nuru iliyotoka mbinguni. Uhasama hasa kwa mitume hutokana na wivu. Mara nyingine wanatambua kwamba wanakaribisha ghadhabu ya Mwenyezi Mungu kwa kuwapinga mitume. Ni wivu wao tu ndio unaowatumbukiza katika kisima cha laana. Ndiyo maana viongozi wa Kikristo, Wayahudi, Wapagani wakati wa Mtume Muhammad

Endelea uk. 3



Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Mwezi Mtukufu wa Ramadhani

Na Ustadh Khamis Sultan Wamwera, Dar es Salaam

Mwanzoni mwa mwezi Agosti 2011, kwa fadhila za Mwenyezi Mungu na rehema zake, Alhadulilah tumeingia katika mwezi mtukufu wa Ramadhani. Ule mwezi wa baraka na neema nyingi kwa waaminio, ni mwezi khalisi wa kuvuna thawabu na kujisogeza hadi kuwa karibu kabisa na Mwenyezi Mungu. Ibada ya swaumu ya mwezi mtukufu wa Ramadhani, inawakutanisha Waislamu wote wa ulimwengu. Kwa hiyo, inatupasa tumshukuru Allah, Alhamdulillah, bali tumuombe atupe afya njema na uwezo wa kutimiza amri yake hii. Amin

Japokuwa makala haya yanawalenga Ansarullah, lakini maudhuwi yaliyomo ndani humu, yanamgusa kila mmoja ajiitaye Mwislamu. Kufunga swaumu si jambo geni kwa wanadamu. Manabii na watu wa dini zote zilizotangulia kabla ya Islam, nao pia walitimiza ibada hii. "Enyi mlioamini, mmelazimishwa kufunga saumu kama walivyolazimishwa wa kabla yenu ili mpate kumcha Mungu" (Suratul Baqara Aya 184). Dini ya Islam inatamka kusudi la kutekeleza ibada hii ni kumcha Mwenyezi Mungu, Mola wa ulimwengu.

Hapana shaka ni bahati njema kwa watu wa ulimwengu huu, kufikiwa kwa mara nyingine na mgeni huyu wa heshima na utukufu, mwezi wa Ramadhani. Ni katika mwezi wa Ramadhani, Kurani Tukufu ilianza kutemremshwa. Ni mwezi mteule wa maombi. Siye tuliokula chumvi nyingi, haikosi tumezowa dhambi kibao, katika mwezi huu, tumuombe Allah Atughofirie. Kwa rehema na huruma yake atusamehe makosa yetu. Maombi tuyafanye kwa moyo wa dhati na yakini kwamba Anayeweza kughofiri na kusamehe madhambi hayupo ila Subhana Wata'ala. Pia tunapoomba msamaha kwa

Endelea uk. 2

Mama wa Khalifa Mtukufu - afariki Dunia

Na Mwandishi wetu

Kwa masikitiko makubwa, tumepokea taarifa za kifo cha Hadhrat Sahibzadi Nasira Begum - mama mzazi wa Hadhrat Khalifatul Masih V. a.t.b.a. ***Inna lillahe wa inna illahe raji'uun.*** Hadhrat Sahibzadi Nasira Begum, aliyezaliwa mwaka 1911, alikuwa ndiye binti mkubwa wa Hadhrat Muslih Maud r.a. na ni mtoto wake wa pili. Mama yake ni Syedda Mahmooda Begum sahiba ambaye naye alikuwa ni binti wa Dr. Khalifa Rasheeduddin. Ndoa ya mama huyu mchamungu ilifanyika mwaka 1934, na baba yake Hadhrat Khalifa wa Pili r.a. alitoa hotuba ndefu. Baba yake, Hadhrat Khalifatul Masih r.a aliweka msisitizo maalum juu ya elimu yake ya dini na dunia na alifikia kiwango cha FA (Advanced level). Tarehe 17 March 1925 ilipofunguliwa Madrssa Ahmadiyya Qadiani yeye akawa miongoni mwa mabinti wa mwanzo kujiunga na Madrassa hiyo. Alifanikiwa vizuri na akapata hadhi ya "Maulvi" mwaka 1929. Kwa kipindi kirefu mama huyu ameshika nafasi ya kuwa Sadr Lajna na sawa na taarifa kutoka kwa akina mama wengi, mama huyu alikuwa na jazba kubwa sana juu ya malezi na elimu ya akinamama. Muda wote alikuwa na hamu kuona kwamba akinamama wa Kiahmadiyya hasa wale wa Rabwah wanakuwa na viwango vikubwa vya elimu na malezi. Aliweka msisitizo maalum juu ya mavazi ya Hijab (Purdah). Kuonyesha jinsi alivyojali mavazi, Hadhrat Khalifatul Masih IV r.h katika hotuba yake ya kwanza (akiwa Khalifa) ya Jalsa kwa akinamama alitaja kwamba anaye dada yake (mama huyu) ambaye yuko makini sana katika suala la mavazi. Akiwa Sadr wa Lajna wa Rabwah alikuwa na hamu kubwa kwamba akinamama wa Rabwah wawe wa kwanza kuliko Jamaat zote zingine

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

MAPENZIYANCHINI SEHEMU YA IMANI

Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. ambaye mafundisho yake ni makamilifu na yanayojibu kila shida ya mwanadamu ametufundisha kwamba **"Mtu kupenda nchi yake ni sehemu ya imani".**

Usemi huu una bahari ya hekima ndani yake; miongoni mwa hizo ni:
Mtu awe na mahaba na ghera ya taifa lake kwani ndio mama yake mzazi, hivyo awe tayari hata kuutoa uhai wake kwa ajili ya taifa lake.
Mtu ajali sheria za nchi yake na kuwa mtiifu kwa uongozi wa nchi yake.
Taifa linafanywa na watu, basi mtu awaone watu wa taifa lake wote kuwa ndugu zake na awe tayari kushirikiana nao katika shida na raha za taifa.
Mtu aelewe kwamba raslimali za taifa lake ni hazina ya wote na hivyo aitunze na kuitumia kwa faida ya taifa lote.
Mtu anapokabidhiwa dhamana ya kusimamia jambo lolote la taifa lake basi aifanye kwa uaminifu wake wote na nguvu zake zote akielewa kwamba kufanya hivyo ni sehemu ya kutimiza majukumu yake kwa muumba wake.

Kwa mtazamo huu basi, si ajabu pia Khalifa wa Pili wa Masihi Aliyeahidiwa, Hadhrat Muslih Maud katika ahadi za viapo vya wana Tanzeem mbalimbali ndani ya Jamaat Ahmadiyya akaweka pia sharti la mwanajumuiya kuitumikia nchi yake kwa uaminifu na utii mkubwa.

Mapenzi kwa taifa ni suala muhimu sana, na ingawaje jambo hilo halikusudiwi kukuza na kuendekeza ukabila bali linakusudiwa kuzalisha ghera ya kuyatumikia mataifa yetu, bila ya mapenzi kwa taifa mtu hawezi kupata nguvu ya kutosha kujasiri hata kuyatoa maisha yake mathalan wakati wa vita, kwani mapenzi ndio nguvu kuu kuliko zote za maungano miongoni mwa wanadamu.

Tuangaliapo historia ya mataifa ni wale tu waliokuwa na mapenzi na taifa lao ndio walioweza kupiga hatua mbele za ufaulu. Watu waliopoteza mapenzi na ghera ya taifa lao, si ajabu kuwa kama yule mjinga akatae tawi alilolikalia.

Leo katika nchi yetu ya Tanzania tunaweza kusema bila woga kwamba kama kuna jambo linaloonekana kupotea katika taifa hili basi ni kutokuwa na mapenzi nalo.
Kwa mdomo tu wengi tunajidaia utanzania wetu na kwamba tunaipenda nchi yetu, lakini majigambo hayo huishia hapo hapo tu kwani linapokuja suala la kuonesha kwa matendo kulipenda taifa letu ni adimu kumkutia Mtanzania anayeonyesha kwa upana kwamba analipenda taifa hili.

Ni wangapi kati yetu tuliokabidhiwa madaraka ambao tuko tayari hata kuliangamiza taifa letu ilimuradi tu tumepata vijiasilia 10 vya kuwekeza miradi yetu na ya jamaa zetu?.

Ni watanzania wangapi leo walio na moyo wa kuona kwamba ni bora kufa kuliko kulisaliti taifa letu na watu wake?

Ni watanzania wangapi leo walio tayari kuwaona watanzania wenzao kama ndugu zao wa mama mmoja?.

Ni Watanzania wangapi wapo tayari kutoa machozi wanapoona Taifa likiwa gizani kwa sababu ya mgao wa umeme?.

Ni Watanzania wangapi wanapata kizunguzungu kwa kuona mashirika yetu yakididimia siku hadi siku na kuuzwa kwa bei ya kutupwa?.

Ni Watanzania wangapi wanaona fahari na uzalendo kulipa kodi ili kuendeleza Taifa letu.

Wakati tunasherehekea nusu karne ya uhuru wa Taifa letu hatuna budi kutafuta na kutafakari juu ya maswala ya hapo juu yaliyoulizwa ili tupewe na Mwenyezi Mungu uwezo wa kuyajibu kwa hekima na busara.

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Wabariki watoto wa Tanzania.

Mwezi Mtukufu wa Ramadhani

Kutoka uk. 1

Mwenyezi Mungu, tusiwe na mpango wa kurejea kutenda dhambi hizo tena. Bali tunatakiwa tusonge mbele katika wema na ucha Mungu.

Hebu kwanza turejee nyuma. Huu ni mwezi mtukufu wa Ramadhani. Tunatakiwa tufanye mabadiliko ya nafsi. Ni lazima tujibadili tuendane nao sambamba. Tufunge swaumu kama mafundisho ya Islam yanavyoeleza, wala tusitwae fikra na mawazo ya watu, tukayafanya ndiyo dira. Mtukufu Mtume wetu Muhammad (s.a.w) amewaambia Waislamu wasichelewe kufuturu. Jua linapozama na kufahamika sasa kumekuchwa mara moja watu wafuturu.

Mmalizapo kuswali swalatul-Maghrib na Isha, daku msile saa 6 au saa 8 usiku umeingia, kama ni hivyo inatupasa kulala. Lakini kabla ya kulala, tunafundishwa na Islam kwamba kwa akali tunatakiwa tufanye mambo haya yafuatayo:-

Kwanza tujitayarishe kuwa na udhu, halafu tuswali rakaa mbili au zaidi za nafali. Katika swala hii, tumuombe Mwenyezi Mungu msaada wa sisi tuishi katika mazingira mazuri ya Kiislam. Tumwambie aendelee kutuepusha na shari za mahasidi wanaohusu nyakati za usiku.

Tukimaliza ibada hiyo, sasa tunaweza kwenda kulala. Tulale, bali kumradhi, tusilale uchi, tuvae nguo ijapokuwa ni nyepesi. tulale kibavu, tena tulalie ubavu wa kulia. Tusilale chali wala tusilalie tumbo. Imesemwa kuwa mlalo wa kulalia tumbo ni mlalo wa watu wenye ashki kubwa na tamaa nyingi sana na ni watu wa motoni. Lala kama tulivyoeleza uwapo juu ya kitanda twayari sasa kwa kulala, soma duwa hili "Allahumma Bismuka amuutu wa ahyaa", yaani Ewe Mola wangu kwa jina lako nafa na kuwa hai.

Tumalizapo kuomba duwa hili, tuendelee kumuomba Allah Atuepushe katika shari ya giza la usiku na katika shari ya wale wanaopulizia mafundoni na katika shari ya wasiwasi wa shaitwani aendae kisirisiri kwa hila.

Ni mwezi mtukufu wa Ramadhani huu. Tusilale lepe wala kipopopo. Aslani tusilale fofofo. Kuanzia nusu ya usiku au zaidi kidogo, tunatakiwa tuzinduke kwa ajili ya ibada ya swala ya Tahajudi. Tumehimizwa na Kurani Tukufu kuwa wakati wa usiku tuamke na tumsudue Allah na tumtukuze wakati mref (Sura Addahr aya 27). Ni ibada ambayo si faradhi, lakini Mwenyezi Mungu Ameisisitiza tuitekeleze, bali Ametamka kwamba Atawapa hidaya wale wote watakaofuata maagizo yake haya. Zawadi aliyowaandalia waja wake hao ni kwamba huenda Akawainua kwenye madaraja ya juu. Basi tusiiachie nafasi hii ipotee bure, tuifanyie kazi. Katika swala hii, tumlilie Mola Atupe maendeleo ya kiroho na dunia. atuzidishie nguvu na moyo wa kuitumikia dini yake ipasavyo.

Tumalizapo swala hii ya Tahajudi, tutayarishe sasa daku. Tumeamrishwa na Islam kula daku katika sehemu ya mwisho wa usiku na kuacha kula wakati wa kupambazuka unapokaribia. "Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu uzi mweupe katika uzi mweusi wa alfajri, kisha timizeni saumu mpaka usiku" (Sura Al-Baqara aya 188).
Tuamkapo asubuhi, tunatakiwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kisha tusome duwa hili "Alhamdulillahi lladhiil ahyaanaa ba'ada maa amaatanaa wailaihi Nnushuur" Yaani, sifa zote njema ni za Mwenyezi Mungu Ambaye Ametuhuwisha baada ya kutufisha na kwake ndiko marejeo.

Tujitayarishe kwa ajili ya swalatul fajri. Tuishilizapo kuswali swala ya asubuhi, tusome Kurani Tukufu, kwa sababu kuisoma Kurani Tukufu alfajri kunakubalika sana. Ni vyema kama kila siku itasomwa juzu moja. Kila kutwa ya mwezi mtukufu wa Ramadhani, tuwe na huzuni kubwa juu ya makosa yetu tuliyoyafanya. Tuwe katika hali ya mtoto mdogo anayemlilia mamaye mzazi. Tuwe na majuto ya kweli moyoni mwetu na huzuni isiyo kifani juu ya makosa na madhambi yetu. Tujiombee elimu na maarifa ya dini. Hatuna tukijuwacho ila kidogo tu. Tumuombe Mwenyezi Mungu Atupe busara na hekima. Katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, tutowe sadaka kwa wingi sana. Tuwasaidie wasiojiweza ili nao waweze kutimiza kufunga saumu ya mwezi mtukufu wa Ramadhani. Furaha yetu kubwa sisi ni kuona wanadamu wote wa ulimwengu wanaongoka na wanasalimika na maafa ya tufani. Tumuombe Mwenyezi Mungu hao wote Awaingize ndani ya safina asibakie hata mmoja nje ya chombo hiki. Hii ni safina ambayo imeundwa na Mwenyezi Mungu Mwenyewe na kumkabidhi Nahodha Mjumbe wa zama hizi Seyidna Ahmad (a.s). Tuwaombee wale wabishi na wakaidi, wasichochee hasira ya Mwenyezi Mungu ikaangukia juu ya ulimwengu.

Naam, leo tunaona vita sehemu mbalimbali ya dunia. Matetemeko, gharika, njaa na magonjwa ya kila aina yametapakaa na kuenea kila janibu. Ajali nyingi zinatokea barabarani, baharini na angani. Watu malaki kwa mamilioni wanaangamia! Kuwapi kwenye usalama? Mashindano ya wao kwa wao ya uundaji wa silaha kali, kama vile Nulear unaendelea kwa kasi ijapokuwa mataifa makubwa yanajaribu kuzuia. Hali ni mbaya, dunia i gharighari. Dunia i ukingoni mwa jahanamu. Ni kwa sababu ya dhambi na maasi ya wanadamu.

Hakuna salama ila tupokee ujumbe wa kweli wa Seyidna Ahmad (as). Sote tutubu dhambi zetu. Kwa mwezi huu mtukufu wa Ramadhani tuwaombee wenzetu wale ambao hadi leo hawajapanda na kuingia katika safina ya Seyidna Ahmad (a.s).

Mama wa Khalifa Mtukufu afariki dunia

Kutoka uk. 1

za Pakistan kwani huo ndio mji wa Khalifa na hivyo isije ikaonekana kwamba "chini ya taa pana kiza". Alikuwa ni mama mwenye uoni mpana sana, aliyependa kushauriana na wenzake na kuwashauri wengine; aliwashauri Lajna wahifadhi beti kadhaa za mashairi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. jambo ambalo liliwapelekea Lajna wa Rabwah kuwa washindi katika '***Bait Bazi***' (mashindano ya kusoma mashairi). Mwenyewe binafsi alihifadhi beti nyingi za Qasida za Masihi Aliyeahidiwa a.s. na kuzisoma mbele ya wanafamilia kila nafasi ilipopatika. Alikuwa ni msomaji wa umakini mkubwa sana wa Qur'an tukufu na pamoja na kuwa na tabia ya kusoma Quran kila asubuhi; muda wowote mwingine uliopatikana baada ya shughuli zake nyingi za kazi za nyumbani na zile za Lajna aliutumia kusoma Kurani Tukufu. Alikuwa ni mama mwenye huruma kubwa na mkarimu kwa wengine na aliyewasaidia wengi kifedha katika matatizo yao mbalimbali. Katika maisha yake yote mama huyu alizama kwenye maombi na mapenzi ya Mwenyezi Mungu kama ubeti wake ufuatao unavyoonyesha.
Mapenzi Yako, Huruma Yako, na Msamaha Wako
Naviombavyotehivyo;Mapenzi Yako daima yanifunike.
Nimepoteza kila kitu kwa ajili ya utii Wake
Ninachohitaji ni msaada wa Mola wangu tu
Nataka Wewe tu uwe rohoni mwangu
Naomba nifunikwe na huruma Yako.

Hadhrat Sahibzadi Nasira Begum alifariki jioni ya Ijumaa tarehe 29/7/2011 na kuzikwa siku ya pili yake huko Rabwah Pakistan. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mama huyu mahali pema peponi. Amin.

Historia ya mama huyu mwema kwa urefu zaidi, itatolewa toleo lijalo. Inshallah.

Nini hasa maana ya Jihad?

Kutoka uk. 1

(saw) hawakuweza kupokea ukweli na hivyo kusimama na kumpinga. Walishughulika sana kuhakikisha kuwa Islam imefutwa kwenye uso wa ardhi. Mwanzoni Waislam walikuwa wachache wapinzani wao katika kiburi na majivuno yao ambao ni desturi na mwenendo wa watu wa aina hii kwani hujifikiria wao wana malinyingi, wanaheshimiwa na wengi. Waliwapa mateso makubwa na makali Masahaba wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Hawakutaka imani hiyo ya Masahaba iote mizizi katika ardhi hii. Walijitahidi sana kuwaangamiza watu hawa wema na hawakupoteza muda hatakidogokatikakuwaongezea mateso. Hofu yao kubwa ni kwamba kukua na kustawi kwa imani hii kungeharibu urua na wafuasi. Wakiwa na hofu hii iliyojaa mioyoni mwao walifanya ukatili mkubwa na kuwaua Waislam wengi bila ya huruma yoyote. Hali hii ya huzuni na mashaka iliendelea kwa takriban miaka 13, wacha Mungu hao walikatwa vipande vipande na jambia za maadui.

Akina mama wasio jiweza na watoto yatima waliuawa mitaani. Bado mafundisho ya Mwenyezi Mungu yalieleza kutolipa ubaya. Na watu wema hao ndivyo walivyofanya, mitaa ilikuwa nyekundu kutokana na damu yao na hata hivyo hawakusema lolote. Walichinjwa lakini hawakulalamika. Mtukufu Muhammad (saw) ambaye sifa zake zinaimbwa huko mbinguni mara kwa mara alipigwa kwa mawe. Mtume huyu mwenye uvumilivu na Istiqama aliweza kupambana na dhoruba hii kwa upole na mapenzi makubwa rohoni mwake. Licha ya uvumilivu na istiqama uhasama uliendelea. Watu hawa wa Mungu walionekana kama nyara. Mwenyezi Mungu Asiyependa watu wabaya ambao ni makatili aliwageukia sasa watu hao wabaya. Hasira yake ilikuwa kubwa. Aliwaeleza watu wake kwa kupitia Kurani Tukufu na Akasemaalikuwaanayaonayote yaliyokuwa yanatendekeka. Siku ya leo Nimewaruhusu kujilinda. Mimi ni Mwenyezi Mungu Mwenye Nguvu. Nitawaadhibu wachokozi. Hii ndio ruhusa iliyotolewa ambayo kwa maneno mengine Jihad. Maneno hasa ya ruhusa yamehifadhiwa katika Kurani Tukufu;

"Imeruhusiwa (kupigana) kwa wale wanaopigwa, kwa saabbu wamedhulumiwa;nakwayakini Mwenyezi Mungu Anao uwezo wa kuwasaidia; Waliotolewa majumbani mwao pasipo haki ila kwa sababau wanasema: Mola wetu ni Mwenyezi Mungu. Na kama Mwenyezi Mungu Asingaliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa mahekalu na makanisha, na nyumba za ibada na misikiti ambamo jina la Mwenyezi Mungu hutajwa kwa wingi. Na bila shaka Mwenyezi Mungu Humsaidi yule anayemsaidia Yeye; Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mshindi" Al-Hajj aya 40 - 41).

Ruhusa hii ilikuwa kwa muda maalum na siyo dawamu, ilikuwa ni ruhusa ya wakati ule ambapo wale walioingia katika Islam walipochinjwa kama kondoo. Kwa masikitiko makubwa baada ya kipindi cha Mtukufu Mtume Muhammad (saw) na Makhalifa wake dhana ya jihad ambayo imejengwa kwenye aya hiyo hapo juu ilipotoshwa. Kuua viumbe wa Mwenyezi Mungu ilifikiliwa kuwa ni sehemu ya imani. Ni jambo la uchungu ya kwamba Wakristo walifanya kosa kuhusu Muumba wao na Waislam wakafanya kosa kuhusu viumbe.

Katika dini ya Kikristo mtu mnyenyekevu na mpole amepewa uungu. Kwa kufanya hivyo shani na utukufu wa Allah uliyoko mbinguni na ardhini umekanyagwa. Na Waislam wameleta maumivu kwa kutumia upanga na mauaji hayo kuyaita Jihad. Wakristo walitumia njia moja ya maudhi, na Waislam wakatumia nyingine.

Ni jambo la kusikitisha kuona ya kwamba makundi yote haya mawili wanajiona wanatenda sawa sawa. Makundi haya yanasikitisha katika hayo wanayoyaamini. Na wanaamini ya kuwa itikadi yao hiyo itawafikisha peponi. Na hakuna jambo jingine linaloweza kuwafikisha peponi isipokuwa kwa njia hizo. Kwa Wakristo uungu wa Yesu na Waislam Jihad. Ingawaje ni dhambi kubwa kumshirikisha Mwenyezi Mungu sitaki kuzungumzia jambo hilo hapa. Ninalotaka kuzungumzia ni dhuluma inayofanywa na Waislam dhidi ya binadamu.

Inatakiwa ifahamike bayana kuwa dhana ya Jihad kama inavyofafanuliwa na maulamaa wa Islam si sawa sawa. Matokeo yake wanamfanya binadamu kuwa mwanadamu mwenye munkar na kumuondolea khulka njema. Na hili hasa ndilo lililotokea. Nina imani damu hii inayomwagika inamwagwa na wale wasiojua sababu ya vita vile vya kwanza vya Islam na hii inatokana na Maulamaa ambao siku zote wanahubiri fikra potofu na matokeo yake ni umwagaji wa damu. Mbele ya viongozi wanaonyesha unyenyekevu kana kwamba wanataka kusujudu, lakini wanapokuwa na watu wa kawaida wanasema hii nchi ni nyumba ya vita - Daarul Harb. Katika nyoyo zao wanaamini kuwa Jihad ni jambo la lazima. Ni wachache tu wanaokataa lakini wengi wanakubali. Wanasisitiza sana juu ya dhana hii ya Jihad, kiasi hiki ya kwamba wanakwenda kinyume na mafundisho ya Kurani Tukufu na kiasi hiki ya kwamba kila anayekwenda kinyume na fikra zao anaitwa Dajjaal na anayestahili kuuawa.

Mimi pia nipo chini ya hukumu hiyo ya kuuawa kwa muda mrefu sasa. Baadhi ya Maulamaa wa nchi hii walinitangaza mimi kuwa Dajjaal na kafiri. Hawakujali sheria za Kiingereza. Wakasambaza fat'wa ya kwamba ninastahili kuuawa. Kuharibu mali zangu na kuwateka wake zangu walitangaza kwamba ni jambo la ucha Mungu kwao. Ni nini ilikuwa sababu ya yote haya? Ni kwa sababu ya mimi kuwa Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi ambaye waliweka matumaini makubwa katika ujaji wake kwani walitarajia atakuja kuvamia na kupora. Na hili ndilo chimbuko la uhasama wao. Lakini inabidi watambue kwamba dhana ya Jihad wanayoiamini wao sio sahihi. Jambo la kwanza dhana yao hiyo ya Jihad inaua huruma. Rai yao kuwa Jihad iliruhusiwa siku za mwanzoni na kwa nini iachwe hivi sasa? Si sahihi. Nina majibu mawili kuhusu hili. Kwanza Fikra yenyewe si sahihi, Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) hakuinua upanga isipokuwa kwa wale waliokuwa wakwanza kuinua upanga dhidi yake. Waliwaua wanaume na wanawake na watoto wasio na hatia kwa ukatili mkubwa sana. Waliua kwa ukatili kiasi hiki ya kwamba machozi hutiririka yanaposimuliwa mauaji hayo. Pili hata kama dhana ya Jihad ni kama inavyofikiriwa na Maulamaa hawa haiwezi kutumika kwa wakati tulio nao. Kwani imeandikwa ya kwamba wakati wa ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa vita vya upanga na vya kidini vitakwisha. Ni dhahiri Masihi hatatumia upanga ama silaha zozote za kidunia kwani silaha yake itakuwa maombi. Istiqama ndiyo itakuwa silaha yake. Ataweka jiwe la msingi la mapatano na kuwaleta pamoja wale wenye munkari na wapole. Zitakuwa ni zama za kuunganika pamoja huruma na mapenzi. Lakini tazama kwa nini wasifikiri kwamba miaka 13 eluf iliyopita Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) alitumia lakabu Yada-ul-Harb kumhusu Masihi Aliyeahidiwa? Hii ina maana kudhihiri kwa Masihi vita vitakoma. Na Kurani Tukufu inatueleza katika hilo;
"Basi mnapokutana (vitani) na wale waliokufuru wapigeni shingo mpaka mmewashinda, kisha wafungeni sana, tena waacheni kwa ihsani au kwa kujikomboa, hata vita vitue mizigo yake. Ndivyo hivyo, na kama Mwenyezi Mungu Angalitaka Angalijilipiza kisasi kwao, lakini Huwajaribu baadhi yenu kwa mikono ya watu wengine. Na wale waliouawa katika njia ya Mwenyezi Mungu basi Hataviharibu kamwe vitendo vyao" (Surat Muhammad aya ya tano).

Tafakari juu kitabu Sahihi-ul-Bukhari (Kitabu kilichokusanya Hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w) na kinachokubaliwa kuwa ni cha pili kwa usahihi baada ya Kurani Tukufu inatakiwa sana tena kwa uangalifu enyi wasomi wa dini ya Islam na nyie wataalamu kuweni makini. Kwa hakika ninasema kweli. Huu sio wakati wa Jihad, msimuasi Mtume Mtukufu wa Mwenyezi Mungu. Masihi tayari amekwishafika na tayari amekwishatoa fat'wa. Kuweni ba'id na silaha zinazotumiwa kumwaga damu. Kutoacha mauaji ya namna hii na kuhubiri dhana hizo za umwagaji damu sio mwenendo wa Islam. Mtu anayenikubali mimi sio tu anaacha kuhubiri dhana hizo potofu bali ataziona kuwa dhana hizo kuwa ni uovu na zinazostahili laana ya Mwenyezi Mungu.

Ningependa kueleza masikitiko yangu kwamba kwa upande mmoja Maulamaa wanakubali maana halisi ya Jihad, lakini kwa upande mwingine wanatayarisha vijana ili wavamie na kuua kwa kisingizio cha jina la Jihad. Na viongozi wa Kanisa wamefanya jambo linalofanana na hilo. Wao wamechapisha magazeti, majarida, vipeperushi katika lugha ya Kiurdu, Pushto, na lugha nyingine wakidai ya kuwa Islam ilienezwa kwa njia ya upanga. Machapisho yao hayo wameyaeneza India, Punjab na sehemu zingine. Matokeo yake ni kwamba ushahidi wa Maulamaa na viongozi wa Kanisa unamfanya mtu wa kawaida aendelee na mauaji ya kikatili.

Katika maoni yangu ni jambo la muhimu ya kwamba serikali yetu ikataze viongozi hao wa dini kuhusu uongo huo, kwani hili ni chimbuko la maasi na fujo katika nchi. Kwa uongo huu wa viongozi wa dini ya Kikristo hautawafanya watu waache dini ya Islam lakini kutokana na mahubiri hayo watu daima watakuwa wakikumbushwa dhana hii ya Jihad na hivyo kupunguza amani yao. Kudhihiri kwa Masihi Aliyeahidiwa kunawalazimisha Waislam kuachana kabisa na suala la Jihad. Ningelikuwa sikudhihiri, pangekuwepo na kisingizio cha kutoelewa maana ya Jihad, lakini kwa kuja kwangu nyinyi mmekuwa mashahidi juu ya wakati huu. Sasa hivi hamna kisingizio chochote cha kutumia upanga kwa ajili ya mambo ya dini. Mtu yeyote ambaye anatafakari na kusoma hadithi za Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) na Kurani Tukufu ya kwamba njia zinazotuiwa na Maulamaa hawa wajinga za kuleta machafuko katu sio Jihad ya Kiislam. Haya yote ni matakwa yao tu na kutaka kwao kwa pepo dhana ambayo imeenea miongoni mwa Waislam. Nimeshawakumbusha ya kwamba Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w) hakuwa wakwanza kuchukua upanga. Kwa hakika kwa miaka mingi sana aliendelea kuumia na wala hakuwa wakwanza kubeba silaha. Na akaweza kuonyesha uvumilivu ambao hauwezi mtu wa kawaida.

Halkadhalika Masahaba wake walifata mwenendo huu kwani wao walifundishwa kuyabeba mashaka yote na kuonesha uvumilivu. Na jambo hili walilidhihirishambeleyaumma. Walikanyagwa kanyagwa lakini hawakulalamika. Watoto wao walikatwa katwa vipande mbele ya macho yao. Walichomwa kwa moto na wala hawakurudishia maovu hayo. Kuna mtu yeyote anayeweza kuleta mfano wa namna hii kutoka kwa Mitume wengine ambao hawakujibu mapigo wakati ambapo wangeweza na hii kwa sababu tu ya Amri ya Mwenyezi Mungu. Kuna mtu anayeweza kutuonyesha kundi la watu ambao walikuwa na uwezo na nguvu lakini kwa miaka 13 wakaendelea kuwa wahanga wa ukatili wa watu waliokuwa wanamwaga damu zao?. Kutochukua hatua yoyote kwa Mtume (s.a.w) na Masahaba zake haikuwa sababu ya udhaifu, kwani ni kweli ya kwamba ni wale wale Masahaba aliyokuwa nao pindi ruhusa ilipotoka ya kupigana Jihad. Mara nyingine watu elfu waliweza kuwashinda jeshi la watu waliokuwa maelfu. Nia hasa ilikuwa ni kuudhihirishia ulimwengu kwamba uvumilivu wao katika mji wa Makka haukutokana na udhaifu ama

Endelea uk. 4

Nini hasa maana ya Jihad?

Kutoka uk. 3

uzembe. Waliumia na kuteswa na kuweka silaha zao mbele ya MwenyeziMungunakuumizwa vilivyo na kuchinjwa kama kondoo kwa hakika uvumilivu wa namna hii ni zaidi ya uwezo wa binadamu.

Tunaweza kuitazama historia ya binadamu na Mitume, mwanzoni kabisa mwa ujaji wa Nabii panaonyesha udhaifu, lakini ukweli ni kwamba watu hao mashujaa wanateswa, watoto wao wanauawa na wala hawajibu hii yote ni kwa sababu ya kusubiri amri ya Mwenyezi Mungu. Na huu ndio ushujaa ulionyeshwa katika miaka 13 na Masahaba wa Mtume Mtukufu Muhammad (sa. w). Ushujaa huu wa kusubiri kwa miaka 13 hapana shaka hauna mfano katika historia ya binadamu. Na kama kuna mtu yeyote mwenye shaka na hili ninalolisema basi atupe mfano mmoja wa hao Waaminio waliopita wa zamani.

Ni vizuri kukumbuka ya kwamba wakati wa mateso haya, Masahaba wa Mtukufu Mtume Muhammad (sa. w) hawakutoa rai yoyote ya kujaribu kukimbia au kuepa mateso haya. Mtume (saw) alichowaomba siku zote ni kuonyesha uvumilivu. Na mtu yeyote aliyeonyesha kutaka kupambana alikatazwa. Mtume (saw) alisema nimeamuriwa kuwa mvumilivu. Mpaka ruhusa ilipotolewa ya kujilinda, Mtukufu Mtume (saw) aliendelea kuhubiri uvumilivu. Hebu jaribu kutafuta uvumilivu wa namna hiyo hivi leo.Au jaribu kutafuta uvumilivu wa namna hiyo kutoka kwa wafuasi wa Mussa (as) au wafuasi wa Yesu (as). Kwa ufupi Waislam wana mfano mzuri sana wa uvumilivu, khulkha njema, na kuacha maovu. Ni jambo la kusikitisha mno na ni bahati mbaya ilioje kwamba vitu hivi vya thamani vimeachwa. Maulamaa wajinga Mwenyezi Mungu Awaongoze wamedanganya umma katika njia nyingi, na uongo huu umeelezwa ya kwamba malipo ni mbinguni. Huu ni uongo dhahiri, huu unakwenda kinyume kabisa na fikra za kibinadamu. Mtu anatembea katika mtaa akishughulika na biashara zake mara nyingine hata hatumfahamu wala hatufahamu jina lake, wala yeye hatufahamu sisi lakini tunamvamia na tunamuua je hii dalili ya taqwa. Hii ndiyo taqwa(uchaMungu) yenyewe? Basi kama hii ni taqwa basi wanyama ni bora kuliko binadamu. Sifa zote njema ni kwa Mwenyezi Mungu. Wale kwa kweli walikuwa ni Wacha Mungu na waliojaa nuru. Mwenyezi Mungu Aliwaamuru kutolipa mabaya hata kama waliporaruliwa.

Kwa amri hii wakawa kama watoto ambao hawana madhara yoyote na wakawa wapole. Kana kwamba mikono yao haikuwa na nguvu na kwamba mifupa yao haikuwa na uwezo wowote. Wengine waliuawa katika njia mbaya kabisa miguu yao miwili ilifungwa kwenye ngamia wawili na ngamia hao walielekezwa katika njia tofauti. Walikatwa katwa kama mboga kwa bahati mbaya kabisa Waislam kwa ujumla na hususan Maulamaa hawajali tena matukio haya. Wao dunia yote wanaona ni ngawira kwao. Kama vile muwindaji anavyotafuta mnyama msituni na kumfuata taratibu na kwa hekima na hatimaye kumpiga huo ndiyo mwendo wa Maulamaa wetu hivi leo. Somo la utu na ubinadamu bado halijawafikia. Wao kumuua mtu yeyote huo ndio Uislam. Wako wapi basi wanaoweza kuonesha uvumilivu wakati wanaonewa kama walivyofanya Masahaba wa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w)?.

Je tumeamrishwa na Mwenyezi Mungu kuwashambulia bila sababu yoyote ama ushahidi wakati hata hatuwafahamu na kuwakatakata na kuwapiga risasi? Je inawezekana ya kwamba imani ya namna hiyo iwe imetoka kwa Mwenyezi Mungu? Imani inayowaua raia wasio na hatia? Kweli tendo hili linaweza kukupeleka peponi? Mtu ambaye hatumfahamu wala hatuna ugomvi naye ananunua bidhaa kwa ajili ya wanae ama anajifanyia kazi yoyote nyingine sisi tunampiga risasi na kwa kufanya hivyo tunamfanya mke wake kuwa mjane wanae kuwa yatima na nyumba yake kuwa mahali pa kilio. Ni aya ipi ya Kurani Tukufu inayowaamrisha kufanya hivyo, na ni hadithi ipi ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) inayowaruhusu kufanya hivyo? Je kuna Maolvu yoyote menye jibu la masuala haya? Wajinga hawaelewi katu Jihad ni nini? Wanatumia dhana hii kwa matakwa yao machafu na dhamira yao ya kumwaga damu.

Nimekwishaeleza kwamba wakati wa Mtukufu Mtume Muhammad (saw) na Masahaba zake, wakati Islam ilipotumia upanga kwa ruhusa kutoka kwa Mwenyezi Mungu ilikuwa ni wakati ule Waislam wengi walikuwa wamekwishauawa na hivyo Mwenyezi Mungu Akaamuru ya kwamba wale wanaoua kwa upanga nao wauawe kwa upanga. Mwenyezi Mungu ni mwenye huruma sana, Mwenye hekima na Mvumilivu, lakini ni Mungu pia wa Wacha Mungu. Inanishangaza kabisa wakati hakuna mtu yoyote anayemuua Muislam kwa ajili ya imani yake, sasa ni kwa sababu ipi na amri ipi wao wanakwenda kuwaua watu wasiokuwa na hatia? Kwa nini Maulamaa hawa wasiwakataze watu hao ambao wanalichafua jina la Islam? Chini ya Serikali ya Kiingereza Waislam wanaishi kwa amani. Wapo wengine ambao waliishi chini ya Serikali ya Kisingasinga wao ndio wanaoweza kueleza sasa hali yao na hal ya imani yao wakati huo. Utoaji wa adhana jambo ambalo ni muhimu katika Islam ilikuwa ni kosa la jinai. Hakuna mtu yoyote ambaye angethubutu kutoa adhana bial kupambana na mishale ya Masingasinga. Si ndiyo maana Mwenyezi Mungu Aliwatoa Waislam katika mikono ya madhalimu wa Kisingasinga na akawaweka chini ya Serikali ya Kiingereza ambayo inaruhusu uhuru wa kuabudu. Kufuatia serikali hii ya Kiingereza Waislam wanaoishi Punjab ni kana kwamba wameipata upya imani yao, na kwa sababu malipo ya wema ni wema hatuwezi kuacha kuwaombea wale waliorudisha amani na kuondoa mateso hayo.

Kwa wale wafuasi wangu ambao wanaamini katika ujumbe wangu, ninawaomba wawe baidi kabisa na uchafu wote huo. Mwenyezi Mungu Amenituma katika nyayo za Masihi Mwana wa Mariam na kunifanya Masihi Aliyeahidiwa. Hivyo ninatangaza muwe mbali na uovu na muwe na huruma na binadamu. Safisheni nyoyo zenu na husuda na temeni sumu chafu na mtakuwa kama malaika. Ni imani ya hovyo mno ambayo haina huruma na mapenzi kwa binadamu. Ni njia mbaya mno iliyojaa miiba na ubinafsi. Enyi nyinyi mlio pamoja nami jivueni na uchafu huo. Tafakari sana juu ya jambo hili - Nini hasa shabaha ya dini? Je ni kuwatesa watu wengine? Hapana -Dini ni njia inayomuelekeza mtu kwa Mwenyezi Mungu, mtu hawezi kumfikia Mwenyezi Mungu na wala hakuna ambaye amewahi kufanikiwa hadi amefanikiwa kuzielewa sifa za Mwenyezi Mungu. Tafadhalini sana kuweni wenye huruma kabisa kwa kila mtu, nifuateni mimi na nitawaonyesha njia mtakapopata imani ya kweli itakayowafanya muwashinde watu wengine. Achaneni na roho mbaya na muwe mbali sana na mambo ya wivu.

Muwe na huruma kubwa sana kwa binadamu na muwe karibu sana na Mwenyezi Mungu. Safisheni nafsi zenu. Ni kwa njia hii miujiza itaanza kutokea. Sala zako zitapokelewa na Malaika watateremka kutoka mbinguni ili kukusaidia. Hii si kazi ya siku moja, anza kupiga hatua na nenda mbele. Jifunze kutoka kwa Madobi. Kwanza anafua nguo yake kwa maji ya moto, anaendelea kufua hadi uchafu unatoka kutokana na joto la maji. Halafu anapeleka nguo hizo kwenye jiwe na kuanza kuzipiga na jiwe na uchafu ule amabo ulikuwa ni sehemu ya nguo unaanza kondoka. Na anaendelea kufanya hivyo mpaka nguo inakuwa safi kabisa. Hii ndio njia ya kusafisha nafsi ya mtu na wokovu wako unategemea na kujisafisha kwa aina hiyo. Na hii hasa ndivyo Anavyosema Mwenyezi Mungu katika Kurani Tukufu; "Nafsi ile imeokolewa iliyosafishwa na uchafu wote na takataka" (Al-Shams, 10).

Nimekuja kwenu na amri. Sasa ni mwisho wa Jihad kwa kutumia upanga, lakini Jihad ya kusafisha nafsi zenu inaendelea. Na hili jambo sio kwamba nimelibuni. Haya ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Jikumbesheni hadithi ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) iliyomo katika sahihi Bukhari ambapo pameandikwa katika mnasaba wa Masihi Aliyeahidiwa Yada 'ul Harb. Masihi Aliyeahidiwa atakomesha mapigano yote ya kidini. Hivyo nawaamuru wote amba o ni wafuasi wangu kujiweka baidi na dhana za namna hiyo. Safisheni nafsi zenu na shindaneni katika usafi wa mioyo na kuonyesha huruma kwa walio dhaifu. Enezeni amani duniani na imani yetu itashamiri. Msishangae haya yatatokeaje. Mwenyezi Mungu Ametengeneza kila kitu hapa duniani bila ya kuhitaji msaada wowote ule. Ametengeneza gari la moshi kukimbia kuliko farasi. Halikhadhalika kwa ajili ya mahitaji ya kiroho Atawatumia Malaika waliyoko mbinguni bila msaada wa binadamu. Alama za kimbinguni zitadhihirika na nuru itaangaza na macho yote yataona nuru hiyo. Hatimaye watu wataelewa kwamba miungu wadogo ambao sio Mungu wametengenezwa tu kwa makosa. Hivyo kaeni ange na uvumilivu. Mwenyezi Mungu Anawivu zaidi na Umoja wake kuliko nyinyi. Jitupeni katika sala ili usihesabiwe miongoni mwa wale wenye kibri. Sikieni nyinyi mnaotafuta ukweli hizi ni siku zilizoahidiwa. Mwenyezi Mungu Hatachelewa kwa muda mrefu. Ni elimu iliyobayana ya kwamba mwanga ukiwekwa mahala pa juu hufika mbali. Na pakiwepo na radi katika sehemu moja ya mawinguni sehemu nyingine pia zinapata mwanga. Hilo litafanyika kwa hivi sasa. Kwani Mwenyezi Mungu Ametoa fursa ya kutimiza bishara hiyo. Kwani ujumbe wa Masihi utaenea duniani kote kama mwanga. Ujumbe huo utaenea pembe zote za dunia kama vile nuru inavyosambaa kutoka mahala palipo palefu (pa juu). Kwa hivi sasa gari la moshi, posta, na njia nyingine za mawasiliano hivi vyote vimeanzishwa ili kutimiza bishara itakayowezesha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa uweze kuenea katika pembe zote za dunia.

Ni kweli ujumbe wa Masihi utafika katika sehemu zote za dunia na utakwenda haraka mithili ya radi katika sehemu zote za dunia. Hivyo kuwepo kwa gari la moshi, posta, pamoja na vyombo vingine vya mawasiliano na kurahisishwa usafiri hizo zote ni alama za ujaji wa Masihi kama ilivotajwa na Manabii wengi. Na Kurani Tukufu inasema "Wa idhal 'ishaaru 'utilati" yaani "Na ngamia watakapoachwa" (Sura At- Takwir aya 5). Kwamba huo wakati wa Masihi atakapodhihiri ngamia watakuwa hawatumiki tena. Njia nyingine za usafiri zitagunduliwa na wakati huo ngamia watakuwa hawahitajiwi.

Katika hadithi Mtukufu Mtume (saw) anasema kwamba ngamia hawatakuwa na matumizi makubwa na kwamba bishara hii haikuelezwa kwa Nabii yoyote mwingine. Hivyo tunatakiwa kutoa shukrani. Yapo matayarisho yanayofanywa mbinguni ya kueneza ujumbe, baraka sasa hivi zimemiminika ardhini. Nyote ni shahidi ya kwamba usafiri umerahisishwa jambo ambalo lilikuwa halijatokea kabla ya. Ni kana kwamba tuna dunia mpya. Matunda yanapatikana hata wakati siyo msimu wake. Usafiri uliyokuwa unachukua miezi sasa hivi unaweza kumalizwa kwa siku, vipo vyombo vingi vilivyogunduliwa vya kurahisisha maisha yetu. Kama ukitaka unaweza kusafiri kwa treni kana kwamba uko katika chumba chako nyumbani. Je hayo sio mapinduzi makubwa hapa ardhini? Kwa hakika hili ni tetemeko kubwa sana ardhini. Mwenyezi Mungu Amekadiria pia mtikisiko hata mbinguni. Hizi zote ni alama za siku za Masihi.

Itaendelea toleo lijalo Inshallah.

بسم الله الرحمن الرحيم

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA TANZANIA - KALENDA YA MATUKIO KWA MWAKA 11/12

MWEZI	MWAKA	TAREHE	TUKIO
JULAI	2011	01-10	Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa – Dar es Salaam.
		11-16	Juma la kukutana na viongozi wa serikali/waandishi wa habari sehemu walipo kwa lengo la kuleta uhusiano nzuri.
		18-23	Wiki maalum ya makusanyo ya michango ya Waqf-e-Jadid na Tahrik Jadid
		22-24	**Jalsa Salana Uingereza**
		31	**Mwandamo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani**
AGOSTI	2011	1-8	Maonyesho ya Kilimo kitaifa - Mikoa husika
		8-15	Wiki maalum ya kuchanga mchango wa mkutano wa mwaka (Jalsa Salana)
		26-31	Siku maalum za Makusanyo ya Eidul Fitri na Eid Fund
		28	Mtihani kutoka kitabu cha: **Saumu ya Ramadhani**
SEPTEMBA	2011	1	**Sikukuu ya Eid Ul Fitri***
		1-10	Juma la maonyesho ya vitabu katika Mikoa husika.
		23 - 25	**Jalsa Salana Tanzania**
OKTOBA	2011	16	Uendeshaji wa semina za Tabligh katika kila tawi.
		22 – 23	**Siku maalum za mahubiri nchi nzima.** Mahubiri yafanyike, viongozi wote wa Matawi ni lazima washiriki, ripoti itumwe Makao Makuu.
NOVEMBA	2011	05-20	Ahadi za Tahrik-e-Jadid kwa mwaka mpya (Novemba 2011/Oktoba 2012)
		8	**Eid Ul Adhha***
		13	Siku ya waanzilishi wa dini. (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii).
		27	Mitihani kutoka kitabu cha: **Hekima ya Mafundisho ya Kiislam (uk. 1 - 47)**
DISEMBA	2011	02-12	Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya Waqf-e-Jadid.
		10 – 11	Ijtimaa ya Ansarullah Kitaifa - Dar es Salaam
		12-18	Wiki ya Tarbiyyat Kitaifa. (Msukumo uwekwe zaidi kwa Waahmadiyya wapya).
JANUARI	2012	09-23	Ahadi mpya za Waqf-e-Jadid kwa mwaka 2012.
		22	Mitihani kutoka Kitabu cha: **Hekima ya Mafundisho ya Kiislam (uk. 48 - 87)**
		23-30	Wiki ya makusanyo ya mchango wa kawaida.
FEBRUARI	2012	01-08	Juma la kuwaalika wageni kwa mazungumzo katika Jamaat zote. Taarifa zitumwe Makao Makuu.
		20	**Siku ya Mwana Aliyeahidiwa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		25-26	Siku maalum za kuwatembelea wagonjwa, mahospitalini na majumbani. Pia kuwatembelea mayatima, walemavu, na vikongwe (washriki, Ansar, Khuddam na Lajna).
MACHI	2012	02-09	Wiki ya kufanya vikao vya kujadiliana ajenda za Shura ya 2012 na kuchagua wajumbe.
		03	**Siku ya Seeratu Nabii.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		10-11	Mahubiri Maalum kwa kila tawi. (Viongozi wote ni lazima washiriki).
		16	Mahubiri ya tarehe 10-11 yatolewe maelezo yake mbele ya Wanajumuiya wote.
		23	**Siku ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii).
		31	Siku ya mwisho ya kutuma dondoo za Mushawara kutoka matawini kwa ajili ya Shura ya mwaka 2012.
APRILI	2012	01	Mitihani kutoka kitabu cha: **Hekima ya Mafundisho ya Kiislam (uk. 88 - 118)**
		6 – 13	Juma la kukusanya malimbikizo ya mchango wa Tahrik-e-Jadid.
		28 - 29	**Shura ya Kitaifa Dar es Salaam – mwaka 2012.**
MEI	2012	07 –14	Wiki ya kukusanya malimbikizo ya michango. (Hasa mchango wa kawaida).
		18	Wajumbe wa Shura wayaeleze matawi yao maazimio ya Shura - 2012
		27	**Siku ya Ukhalifa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii).
JUNI	2012	08 – 15	Wiki ya kuhakikisha kwamba kila Mwanajumuiya amekamilisha Bajeti ya michango yake hasa wa kawaida/Wasia sawa na kiwango cha kila mwezi. Juhudi maalum zifanywe.
		15 – 17	**Ijtimaa na Shura ya Khuddamul Ahmadiyya Kitaifa.**
		23 – 25	**Ijtimaa na Shura ya Lajna Imaillah Kitaifa.**

*Zingatia: Saumu ya Ramadhani, na Sikukuu zote mbili zinategemea kuandama kwa mwezi.

Bustani ya Washairi

UHURU NIUTAKAO

1. Yu Mwema Aso kipeo, Muumba nchi na mbingu
Akajaza vivutio, viumbe kila mafungu
Ninamuomba mkao, nikunjue mbawa zangu
Nibaki kuwa wa Mungu, uhuru niutakao.

2. Uhuru niutakao, nibaki kuwa wa Mungu
Niwe kwenye mtandao, ujazo wa ulimwengu
Mbizi na maogoleo, kina cha fuadi yangu
Nibaki kuwa wa Mungu, uhuru niutakao.

3. Wapi penye kimbilio, pasipokuwa kwa Mungu
Mengine maangamio, nisikize moyo wangu
Shika langu dhamirio, kuridhi Msiri wangu
Nibaki kuwa wa Mungu, uhuru niutakao.

4 Hasa langu kusudio, nikhalisi nia yangu
Amri na makemeo, nitimize kila fungu
Nigawe vyema gawio, nisizidishie kwangu.
Nibaki kuwa wa Mungu, uhuru niutakao.

5. Nibane vyangu vilio, vibaki kwa Mola wangu
Lisisikie sikio, sala na dhikri zangu,
Nimeze kwa gugumio, yalo zidia uchungu,
Nibaki kuwa wa Mungu, uhuru niutakao.

6. Napatwa na mshangao, nionapo walimwengu
Wanyenyekeavyo vyeo, vilivyojaa majungu
Na kupenda machukio, yalo moshi na ukungu
Nibaki kuwa wa Mungu, uhuru niutakao.

7. Yote naona pumbao, yatele kizunguzungu
Nawapande wapandao, wazame kwenye mawingu
Sijali madaha yao, naomba haya ya kwangu
Nibaki kuwa wa Mungu, uhuru niutakao.

8. Mshindo huo ujao, nani mnusuru wangu
Sina ushirika nao, mke na watoto wangu
Rafiki wanifaao, wanikumbushe kwa Mungu
Nibaki kuwa wa Mungu, uhuru niutakao.

9. Wale wang'ang'anio, kupora uhuru wangu
Kuna nini kwangu chao, wakichukue wezangu
Mbona zangu hitajio, akidhie Mola wangu
Nibaki kuwa wa Mungu, uhuru niutakao.

10. Wasia niandikao, si wa leo ni wa tangu
Ila uwapo si fao, niacheni peke yangu,
Nahofu waniitao, ili wanifunge pingu,
Nibaki kuwa wa Mungu, uhuru niutakao.

A. M. Ame

UJIO WA MUBARAKA:

1 Alihamdulillahi, Twamshukuru Manani
Kututumia Masihi, hapa hapa duniani
Ujaji wake Masihi, wa Mola mwenye hisani
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

2 Alitangaza Masihi, Mahadi wake Manani
Mola katupa habari, atafika duniani
Tumpokee tukiri, mkombozi wa insani
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

3 Huyu nasema Masihi, si mwingine wa Muhamadi
Katumwa naye Jalali, kuihami yake dini
Si nyingine hiyo dini, Isilamu nabaini
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

4 Moja tisa ziro nane, kazi yake akanadi
Kalongasi ya kisasa, ni ile ya Muhamadi
Na kaanzisha, Jamia jinale Ahamadiya
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani

5 Chombo cha kuongozea, dini ya Isilamia
Mola Akabarikia, na sasa yaendelea
Vikwazo akaondoa napema kimefikia
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

6 Kaanza tunga kurasa, kupitia Kuruani
Kitabu chenye kurasa, liandika hadharani
Kila kitu aligusa, wasomi pate baini
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

7 Kaeleza hasa hasa, watu walikithamini
Yandani yaliwagusa, ikawafika yakini
Mtego ukawanasa, walilalama jamani
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

8 Kitabu chenye kurasa, zaidi ya themanini
Mashekhe Maprofesa, sifa walizibaini
Kwa ubora wa kurasa, wakayajua ya dini
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

9 Kitabu hicho nasema, kwa jinale Barahini,
Ni mengi aliyasema, ya Isilamu ya dini
Hakuacha hata nyuma, ya kutia mashakani
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

10 Utabiri alipewa, wa mwana atazaliwa
Mwana huyu tazaliwa, kwa baraka za Jalia
Takuwa mwenye kujua, kuhusu Isilamia
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

11 Wahai alifikiwa, kutoka kwake Jalia
Wakuhusu kuzaliwa, kwa mwana mtarajiwa
Shukurani alitowa, kwa wahai kupokea
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

12 Masihi wa Muhamadi, Tarifa alizinadi
Za mwanaye mutaraji, atazaliwa na nadi
Badaya tisa idadi, miaka naibaini
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

13 Na wana wakazaliwa, katika tisa miaka
Hawakuwa wahidiwa, kwa ilivyotarajiwa
Mwongo wakamdhania, kumbe bado yake miaka
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

14 Kwa fadhila za Jalali, na mwana akazaliwa
Fedheha kwa majahili, hakika iliwafika
Wakabaki vichwa chini, aibu zikawafika
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

15 Pinzani kushika kasi, wakimpinza Masihi
Masihi kwa yake kasi, hakika walifedhehi
Wakakosa na risasi, magobole yakafeli
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

16 Ushindi wake Masihi, ukanza kupata hali
Kwa uchache wafuasi, walizijaza bayati
Wakajiunga kwa kasi, kwa mapenzi ya Jalali
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

17 Mwana huyu wa ahadi, elimu kujipatia
Alipata ya akhera, ya dunia kadhalika
Kwa baraka za wadudi, elimu alimjuvya
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

18 Mwana huyu wasikia, Mahamudu Ahamadi
Kajaliwa na Jalia, elimu ya Kuruani
Hakuna wa kuingia, asimamapo jukwani
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

19 Na yake nitayanadi, zamu yake ikifika
Kwa uchache nitanadi, na yale yalotufikia
Kwa zake njema juhudi, wote tumefaidika
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

20 Yote hayaelezeki, kwa vipande nimetoa
Mpate kuyahakiki, akilini kuyaweka
Msome kwa itifaki, kwa uwezo mtojaliwa
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

21 Na sasa nasimulia, baraka za Ukhalifa
Hizi ziliahidiwa, na Mola wetu mpendwa
Kuruani ilotukuka, na humo kaelezea
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

22 Silisila Isilamu, Mtume akitawafa
Nafasi hiyo muhimu, hushika wake Khalifa
Khalifa huyu Imamu, hutumika hadi kufa
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

23 Masihi alipokufa, Khalifa alisimikwa
Alisimikwa Khalifa, wisilamu kukwamua
Wa kwanza wetu Khalifa, Nuru dini nakwambia
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

24 Alijaliwa hakika, Isilamu kutumika
Mbele aliupeleka, kwa baraka za Jalia
Kifo kilimfikia, wa kwanza wetu Khalifa
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

25 Mahamudu Ahamadi, nafasi aliishika
Kwa baraka za Wadudi, Ukhalifa kumfika
Kamchagua Wadudi, Jumuiyya kupeleka
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

26 Mahamudu Ahmadi, jinale naongezea
Ni lake Bashirudini, na mengine jalizia
Umeyapata nadhani, tayari umeyajua
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

27 Khalifa huyu wa pili, naanza kuelezea
Aliifanya juhudi, kwa kufanya ya Jalia
Kazi hii kwa juhudi, hakika alijitoa
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

28 Mipango aliinadi, dunia ipate jua
Akaanzisha mradi, kuisukuma Jamia
Kwa baraka za Wadudi, Mola akaujalia
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

29 Jamani huo mradi, Tahriki ukaitwa
Malizia na Jadidi, manufaa ulitoa
Akapitisha juhudi, kwa kila Ahamadiyya
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

30 Mpango wa Tahriki, mchango ulitakiwa
Kila mwana wa Jamii, aliombwa kuutoa
Mpango huwa Jadidi, kwa wingi walichangia
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

31 Madhumuni naeleza, wa hu mpango sikia
Ilikuwa kwendeleza, ya Mola hii Jamia
Hakika aliikuza, kila nchi ikafika
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

32 Kazi hii ilianza, mchango ulipokuwa
Khalifa alijikaza, wabashiri kuwatowa
Mbashiri kutumwa kwanza, Mubaraka alitumwa
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

33 Na sasa naelezea, ujio wa Mubaraka
Jinsi alivyoingia, Mashariki Afrika
Khalifa alimtoa, Tabora akafikia
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani

34 Na mwaka aliofika, sasa ninakutajia
Ni elfu tisa mia, na thelathini na sita
Ni kijana mwenye rika, hakika aliingia
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

35 Mubaraka aliingia, Tabora kawasilia
Watu walimpokiea, kwa nderemo za sifaa
Madhumuni kuingia, hakusita kuyatoa
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

36 Ujaji wake Masihi, lianza kuelezea
Mpendwa wetu Jalali, tayari kisha mtuma
Ni Miriza Ahamadi, Masihi Mwaahidiwa
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani

37 Mtajika wa Masihi, twatakiwa kumjua
Kuwa yeye wa ahadi, kahidiwa na Jalia
Ndani yake Kuraani, na Hadithi kadhalika
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

38 Watu walisikiliza, kwa tofauti hisia
Na wengine walimbeza, kebehi kumtolea
Hasa alipoeleza, Ni Mtumewe Jalia
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani

39 Kadiri alivyokaa, Mola Alibarikia
Watu walianza jua, Bayati wakaingia
Kuipokea Jamia, na Mjumbe wa Jalia
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

40 Watu walioingia, walikuwamo waesha
Wafirika nao pia, kadhalika limjua
Ni Athumani sikia, mwana wa Kambaulaya
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

41 Rashidi naendelea, ni mtoto wa Bundala
Kadhalika na Yusufu, baba yake ni Dunia
Na Masudi wasikia, Masagala likikaa
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

Endelea uk. 7

Kutoka uk. 6

42 Wengine naendelea, Mzee Simba sikia
Pia ninakutajia, wa Uyui Bwana Musa
Hawa wote nakwambia, Jamia walipokea
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

43 Na wengine wapo pia, majina sintoyatoa
Walijiunga sawia, ndani ya hii Jamia
Ikasitawi Jamia, kwa baraka za Jalia
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

44 Shekhe wetu Mubaraka kidume alisimama
Mipango aliiweka, Msikiti kusimama
Majaliwa ya baraka, waraka aliutuma
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

45 Waraka huo hakika, Bomani aliutuma
Kwa serikali tajika, ya Mwingereza nasema
Na ombi lake hakika, ni kiwanja cha heshima
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

46 Nasema huu waraka, na bomani ulifika
Bwana Pisi mtajika, aliupata hakika
Tafakari aliweka, kutoa jibu haraka
Ujio wa Mubaraka, umetutoa gizani.

47 Na kiwanja alitoa, gongoni kuwapimia
Kuwa hapo ninatoa, ujenzi pate anzia
Ujenzi nawatakia, uwe wa heri sikia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

48 Wahamadiyya sikia, majibu yaliwafika
Majibu kufurahia, yatoka kwa mtajika
Shukurani walitoa, kumshukuru Rabuka
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

49 Ilifuata shughuli, ya ujenzi wa makini
Wa msikiti halali, kwa idhini ya Manani
Wapinzani mafedhuli, walisimama makini
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

50 Walisimama makini, usijengwe msikiti
Mahala hapo gongoni, walikataza kwa dhati

Na vita havina mboni, wakayachana mashati
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

51 Vita hivi nakwambia, vilikuwa ni vikali
Sheikhe wetu wasikia, ikamfika ajali
Maumivu kaumia, katika wake mwili
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

52 Wahamadiyya sikia, walikuwa ni wakali
Wakasimama imara, navita kuvikabili
Ziliwajaa hasira, adui kumkabili
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

53 Asikari walifika, kwenye tukio la ajali
Walishikwa wahusika, walioleta ajali
Mahakamani kufika, hukumu kuwakabili
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

54 Kifungo kuhukumiwa, wapate pata akili
Tena wasijerudia, kwenye jambo kama hili
Sheikhe wetu wasikia, kalazwa hosipitali
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

55 Mubaraka alipona, katoka hosipitali
Huruma yake mwanana, msamaha alijali
Kesi hiyo alikana, kafuta bila kujali
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

56 Hata hivyo wasikia, dhamira ilimwijia
Kiwanja hakutarajia, uwazi kukiachia
Gongoni hapo mahala, nyumba alipendelea
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

57 Nyumba hiyo ikijengwa, itakuwa ya Jamia
Na Shekhe wetu mlengwa, humo apate kalia
Na wote wanaJamia, shauri walipokea
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

58 Kwa fadhila za Jalia, nyumba ikakamilika
Ujenzi ukaishia, wabashiri kufikia
Shukurani kuzitoa, kwa Mola Alojalia
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

59 Mipango mipya kuweka, wapi wapate eneo
Eneo la uhakika, la msikiti kuwepo
Hapo walikusanyika, na kuweka mwelekeo
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

60 Mwelekeo ulikuwa, wakutane na waombe
Wamwombe wetu Jalia, zake baraka Aweke
Maombi walichangia, zikashuka heri zake
Ujio wa Mubarak, umetutoa gizani

Haruni Bundala Tabora

Litaendelea toleo lijalo. Inshallah

TAREKHE YA AHMADIYYA TANZANIA

Kutoka toleo lililopita

896. Hii ni kubwa hisani, kutoka Kwake Manani,
sisi tutasema nini? Twamshukuru Jalia.

897. Tanga bwana, bwana tanga, si ardhi ya wajinga,
watu walo kwenye mwanga, wa elimu ya tangia.

898. Wakristo vijana, wanayo elimu pana,
na dini yao kwa sana, kwa upeo waijua.

899. Wakijadili khabari, watulivu na mahiri,
wala hawaleti shari, ya magomvi na ghasia.

900. Ngoma kwa Waislamu, wanaochpa karamu,
waandika talasimu, na kukana manabii.

901. Hao ndo wa matatizo, ndio waleta mizozo,
ndio waleta chukizo, wengine kuwachukia.

902. Wampaisha mbinguni, yule nabi wa zamani,
na kumrejesha chini, utume kuendelea.

903. Nabii wa Wayahudi, mara ya pili arudi,
wafasi wa Muhammad! Awe wao Masihia?

904. Ajabu kisha ajabu, hayo mnayojaribu,
kueleza yana jibu, au mwajiropokea?

905. Muhammad mwamfisha, kwa maji mnamkosha,
na sanda mnamvisha, kishapo mwamfukia!

906. Isa ananenepeshwa, hakufa amepaishwa,
na kisha atarejeshwa, kuirudia dunia!

907. Ni sawa hayo jamani? Yatoka kitabu ganio?
Injili au Qurani, nasi twapenda kujua.

908. Myaka ya nyuma akali, iliyopita ndo hali,
tanga waliikubali, nao waliyapokea.

909. Kipita barabarani, wajipiga kifuwani,
wakikohoa njiani, si wagonjwa wa kifua.

910. Wao walo wakidhani, kufanya hivyo ndo dini,
kutotenda ushetwani, ndivyo walifikiria.

911. Walivyo wakifikiri, ni hiyo ndiyo dhikiri,
Aloitaja Qahari, kumbe walikipotea.

912. Kwenye hali hiyo hali, Sarwar, Adullah Ali,
ndo Tanga hao wawili, Jamia walitetea.

913. Kabla pali Ayaz, yeye akifanya kazi,
ni mwalimu kiongozi, pale kwenye shule moya.

914. Ni shule ya serikali, bali pia alijali,
dini hakuidhalali, akiitangaza pia.

915. Watu walimtambua, yeye mwana Jumuiya,
akienda kuongea, nao bila ya udhia.

916. Kuja kwa shekhe sarwar, Abdullah Ali Sadiri,
pakaongezeka ari, tabligh kuenea.

917. Watu kisimuliana, na huku wakionyana,
Ahmadiyya kimwona, kusema naye achia.

918. Mirzai Kadiani, wameiritadi dini,
tazameni walakini, wanayo elimu pia.

919. Utadhani Islamu, wanzapo kutakalamu,
wana mtume Ghulam, nabii wao mweshia.

920. Hiyo ndo kauli yao, suni na mashekhe wao,
kisema wao kwa wao, walivyo kisimulia.

921. Ni Muhammadi Ayubu, Tanga kivuma ajabu,
ndiye shekhe kwa hesabu, waliye muhesabia.

922. Waila hakika yake, ali shekhe wa makeke,
achia nidhamu yake, alivyo kitufanyia.

923. Katowa mengi matusi, akitutukana sisi,
ati dini tumeasi, na mengi kutuzulia.

924. Na pia Amiri Juma, naye alikuwa nyuma,
kwa kuileta hujuma, isifaulu Jamia.

925. Na Abdallah Jambeni, hakujilisi pembeni,
alikuwamo kundini, kuipinga Jumuia.

926. Mashekhe watatu hao, pamwe na wafasi wao,
waliweka nguvu zao, kushitiza Jumuia

927. Na sumu ya upinzani, waliingiza nyoyoni,
mwa watu misikitini, Jumuia kuchukia.

928. Waliwambia nisai, tuitwe mamirzai,
walipandikiza sui, isiyokuwa na njia.

929. Waume walinenani, tuitwe Makadiani,
kuongeza tafrani, ya chuki na ya ghasia.

930. Tanga pakawa fukuto, la mahubiri ya moto,
si mkubwa si mtoto, Ahmadiya ajua.

931. Walojuwa ndio hao, ndio hao wasemao,
utume maendeleo, kukoma kujichimbia.

932. Kujichimbia kaburi, mkajizika vizuri,
kwa kweli hii khatari, angalieni sawia.

933. Sisi tunachoamini, Isa kwa msalabani,
hakufa, hakwenda mbinguni, kawaida kajifia.

934. Kule majani mapana, mwalimu wetu kijana,
Ng'ambage alikutana, na watu wakiongea.

935. Na mazungumzo yao, khasa juu ya majio,
ujio wa mtu huyo, anayeitwa Masia.

936. Na mwalimu hakungoja, "Masihi mwenyewe kuja",
na jina akalitaja, "Ahmadi maridhia".

937. Watu: "Astghafiru", ati amesha kufuru,
tusiseme haidhuru, mambo tutayakosea.

938. Mtu mmoja fulani, ajulikana "Majani",
alishika mkononi, Hadidi kumtupia.

939. Alimpiga kwa chuma, kwa hoja alipokwama,
ni nini? Ndio hekima! Sijapata kutambua.

940. Ilimpata kichwani, mwalimu wetu jamani,
kafika sipitalini, pale alipasuliwa.

941. Kapasuliwa kichwani, ni karibu ya jichoni,
hayo ni mafunzo gani, msomaji fikiria.

942. Nini wapinzani nini, kama hamjuwi dini,
msijitie pambani, aibu mtajitia.

943. Bada ya hilo tukio, wakazizidisha mbio,
kuwaendea makwao, si kwa mikwaju; ni Aya.

944. Shughuli za mahubiri, ikazidi kushamiri,
walio watu mahiri, vizuri walipokea.

945. Wapo waloathirika, ukuta wakakiuka,
wakaja kuunganika, Jamia wakaingia.

946. Walojiunga wambele, ni Rashidi Kihaule,
mzee Kombo vivile, Kabasha alifatia.

947. Kajiunga na Baruwa, Ambaye Tanga mzawa,
bin Yusufu akawa, idadi aongezea.

948. Hao wali wa awali, walokubali ukweli,
tarekhi yawanakili, na picha yawachukua.

949. Hao walipojiunga, mahubiri yalisonga,
tuone watu wa Tanga, wapi watakimbilia.

950. Hapakuwapo mchoko, walifatwa huko huko,
ambako huko waliko, khabari kuwaambia.

951. Pakawapo Maulidi, ya Mtume Muhammadi,
na Masuni walinadi, yeyote kwenda sikia.

Itaendelea toleo lijalo. Inshallah

Al-Ustadh Khamisi S. S. Wamwera
Kimbangulile - Mbagala Rangi Tatu,

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq

Kutoka toleo lililopita

UGONJWA

Ushahidi wa tatu ni: Sema: Hakika nayafuata yaliyofunuliwa kwangu kutoka kwa Mola wangu. Hizi ni dalili zitokazo kwa Mola wenu na ni mwongozo na rehema kwa watu wanaoamini. Na Kurani isomwapo, basi isikilizeni na nayamazeni ili mpate kurehemiwa (7:204-205).

Tarehe 10 Februari 1911, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliwaambia wale aliokuwa nao maneno yafuatayo:

"Ni kubwa sana rehema ya Mungu iliyo juu yangu. Ameonyesha nguvu Yake na himaya Yake kwa mtumishi Wake mnyenyekevu kwa njia za ajabu katika siku za maradhi yangu. Nimepata uhakikisho upya kuhusu maombi kupokelewa. Maombi ndiyo njia kubwa sana kwangu kupata hisani Yake. Mola wangu Amenijaalia hisani zake kubwa. Laiti ningekuwa na uwezo wa kuwaambieni kirefu. Leo tu nilifunuliwa: 'Nijaalie kwa fadhili yako nisimhitaji yeyote minghairi yako.' Nilikuwa na shida ya kutopata usingizi. Madaktari wakaninywesha dawa, lakini bure. Usiku uliopita sikutumia dawa, nikalala masaa matano. Mungu Yu Mfalme Mwenye nguvu; Hufanya Apendavyo. Kumbukeni nasaha hii yangu. Muwe na imani katika Mungu, na mtarajie kujipatia fadhili yake. Msivunjike moyo kwa sababu ya kuzikabili shida; hizo zinaletwa kuwanyanyueni. Mwombeni Mungu msaada. Jambo hilo ni dogo tena rahisi lakini ni la muhimu sana. Lizingatieni, msiliachilie mbali. Mungu Awe pamoja nanyi, Awalindeni na kuwahifadhi. Amin."

Mtu fulani alimwuliza Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. tarehe 27 Februari 1911, ya kwamba hitilafu za kiitikadi baina ya Waahmadiyya na wasiokuwa Waahmadiyya ni katika mambo makubwa ya kimsingi au katika maelezo? Akajibu kwamba si sawa kusema kwamba hitilafu hizo zinahusu mambo ya maelezo. Sala yetu ni kama sala yao, pia hamna hitilafu kuhusu zaka, haji na saumu. Naona tuwahitilafiana kuhusu jambo la msingi. Twaweza kueleza habari hiyo kwa njia hii. Imani huhitaji kumwamini Mungu, Malaika Zake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, Kadri Yake njema na mbaya na Ufufuo. Wapinzani wetu pia wanatangaza kuamini hivyo vyote, lakini hapo ndipo hitilafu ianzapo. Mtu hawezi kuwa mwaminio isipokuwa awe anawaamini Mitume wote wa Mungu pasipo kutofautisha baina yao kwa sababu ya zama zao au mahali pao. Kumkataa Mtume yeyote wa Mungu kwamfanya mtu kafiri. Wapinzani wetu wanakataa madai ya Hadhrat Mirza Sahib a.s. kuwa ametumwa na Mungu. Hili halihusiani na habari ya maelezo. Kurani Tukufu yausia: 'Hatutofautishi baina ya mmoja wa Mitume Wake' (2:286). Kumkataa Masihi Aliyeahidiwa kwamaanisha kutofautisha. Twamwamini Mtume Mtukufu s.a.w. kuwa Khatamun Nabiyyin kama alivyoitwa ndani ya kurani Tukufu (33:41). Twaamini ya kuwa asiyemkubali kuwa Khatamun Nabiyyin ni kafiri. Twahitilafiana na wapinzani wetu kuhusu maelezo ya neno hili; lakini hitilafu hii haihusikani na: Hatutofautishi baina ya mmoja wa Mitume wake. Hivyo, naona kwamba kuna hitilafu ya kimsingi baina ya wasiokuwa Waahmadiyya na sisi.

Siku hiyo akamwandikia Nawab Fateh Ali Khan wa Lahore akiahidi kutoa rupia elfu moja katika mfuko wa Chuo Kikuu cha Waislamu, na akatoa maagizo yafuatayo kwa wanajumuiya wa Kiahmadiyya:

"Upo mpango wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Waislamu katika India, na baadhi ya marafiki zetu wameuliza kwamba je, wanaweza kukichangia. Ili kuwajulisha wanajumuiya inatangazwa kwamba ingawaje Jumuiya yetu ina mahitaji maalum na wanajumuiya wanapaswa kuyachangia vya kutosha, hata hivyo, kwa kuwa mpango wa Chuo Kikuu cha Waislamu unafaa, hivyo nafikiri yawalazimu marafiki zetu kukichangia kwa kila njia ili kukisaidia."

Mwanzoni mwa Aprili 1911, gazeti moja la Waislamu la Lahore lilipendekeza kwamba siku ya kuzaliwa Mtume Mtukufu s.a.w. iwe inasherehekewa kama sikukuu, natawiletulaSimlalikamwomba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. mwongozo kuhusu pendekezo hilo. Akajibu:

"Mtume Mtukufu s.a.w. aliweka sikukuu mbili tu kwa Waislamu, na siku ya ljumaa pia kama Idi. Sikukuu yoyote nyingine itakuwa bidaa isiyotakikana. Kwa



Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masih I r.a.

njia hiyo watu wataendelea kuongeza sikukuu nyinginezo. Waahmadiyya pengine watapenda kusherehekea kila mwaka siku alipopokea Masihi Aliyeahidiwa a.s. ufunuo wake wa kwanza na pia siku ya kufariki kwake. Masahaba wa Mtume Mtukufu s.a.w. walikuwa wamejitolea sana kwake, lakini katu hawakusherehekea sikukuu ya tatu. Masihi aliyeahidiwa a.s. alikuwa anampenda sana Mtume Mtukufu s.a.w., kama sikukuu kama hiyo ingeliruhusiwa angelisherehekea. Mapendekezo kama hayo ni ya kijinga, wanaoyaleta hutafuta kupendwa na watu; hawaongozwi na sababu ya kiroho."

Hadhrat Khalifatul Masih r.a. alisalisha sala ya kwanza ya Ijumaa baada ya kupata ajali, baada ya kitambo cha miezi sita. Huo ulikuwa wakati wa furaha kubwa katika Jumuiya nzima. Tangu hapo akaendelea kwa muda mrefu sana kuhudhuria sala ya Ijumaa msikitini, lakini sala zote pamwe na sala za Ijumaa ziliendelea kusalishwa naSahibzadaMirzaBashiruddin Mahmud Ahmad r.a. Wakati fulani Maulawii Muhammad Ali alimshauri Hafidh Raoshan Ali r.a. kwamba amwulize Hadhrat Khalifatul Masihi kwa nini yeye anamwagiza kijana Sahibzada kuongoza katika sala ilhali wapo masheikh walio wazee na wataalamu zaidi. Hafidh Raoshan Ali r.a. aliuliza hilo bila kueleza nani alimwambia kuuliza hivyo, naye akajibiwa:

"KuraniTukufuyasema:Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mungu ni yule amchaye zaidi katika nyinyi" (49:14). Mtaje hata mmoja miongoni mwa Jumuiya nzima aliye mcha-Mungu zaidi kuliko Mian Mahmud Ahmad. Ndipo nitamfanya Maulawii Muhammad Ali awe anaongoza katika sala na kutoa hotuba."

Serikali ya Kiingereza ilitangaza kwamba Baraza la kumvika Mfalme taji litafanywa mjini Delhi tarehe 12 Desemba 1911, kwa kutangaza kutawazwa kwa Mtukufu Geroge V Mfalme wa India. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaona itakuwa nafasi nzuri ya kumwomba Mfalme Mtawala, kwa kumpitia Mheshimiwa Gavana Jenerali wa India, kwamba Waislamu walio wafanyakazi wa Serikali wapatiwe ruhusa ya masaa mawili kila siku ya Ijumaa ili kuwawezesha kushiriki katika sala ya Ijumaa. Kwa shabaha hii akaandika hati ya maombi kuhusu hayo akatangaza tarehe 1 Julai 1911:

"Ijumaa huhesabiwa katika Islam kuwa ni siku iliyobarikiwa sana, na Waislamu wanaiheshimu kama sikukuu. Kuhudhuria katika sala ya Ijumaa ni jambo la lazima na inasisitizwa sana kuliko kuhudhuria katika sala za idi mbili, ilivyosemwa na Kurani Tukufu: Enyi mlioamini, inaponadiwa kwa ajili ya sala siku ya Ijumaa, basi nendeni upesi kumkumbuka Mwenyezi Mungu na acheni biashara (62:10). Ndiyo sababu tangu mwanzo wa Islam, siku ya Ijumaa ni ya ruhusa katika nchi zote za Kiislamu. Katika India pia Ijumaa iliendelea kuwa siku ya ruhusa kwa karne nyingi. Aya iliyotajwa sasa hivi haimruhusu mtu kusali sala ya Ijumaa peke yake; yamlazimu kuhudhuria msikitini, kusikiliza hotuba na kisha kusali nyuma ya Imam pamoja na waaminio wengine.

Jumapili ni siku ya ruhusa sawa na dini ya Mfalme, na shughuli za serikali hazina nafasi ya kutoa ruhusa mbili katika wiki. Kwa hiyo imebidi kutoa shauri itakayotimiza matakwa ya Waislamu pasipo kuzusha matatizo kwa kuendesha mambo ya serikali. Njia moja rahisi itakuwa kufunga ofisi, mahakama na shule zote na vyuo vyote kwa masaa mawili wakati wa sala ya Ijumaa, au kuwaruhusu wafanyakazi na wanafunzi walio Waislamu, kwa muda huo ili waweze kushiriki katika ibada ya Ijumaa. Idara na ofisi zote zaweza kupelekewa barua kuhusu habari hii.

Tumetayarisha hati ya maombi kwa shabaha hii ili kumpelekea Gavana-Jenerali. Lakini kwa kuwa habari hii inawahusu Waislamu wote kwa jumla, hivyo kabla ya kupeleka hati hii, inabidi Waislamu wote, magazeti na vyama viarifiwe ili viiunge mikono kwa njia ya maazimio, matangazo, makala na kadhalika, na serikali ikipata uhakikisho wa haja hii ya Waislamu, iweze kutoa nafasi hiyo. Tunahusika na habari hii kwa njia hii tu ya kwamba kwa kuwa hiyo ni haja ya Waislamu wote, basi ombi lipelekwe ili liungwe mkono na Waislamu wote. Sio utashi wetu kwamba ombi lepelekwe na sisi tu pekee. Jinsi Mungu Alivyotuongoza ndivyo tuliyopendekeza shauri hii. Kama chama chochote cha Waislamu kikikataa pendekezo letu hili kwa sababu tu tumelitoa sisi, hatutalipeleka bali njia nyingine yoyote inayofaa itumiwe kulipeleka hilo serikalini."

Kutoka Aligarh ikashauriwa ya kwamba kumbukumbu iliyopendekezwa itumwe serikalini kwa niaba ya chama cha All India Muslim League. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akatoa kibali chake. Matokeo ya kumbukumbu yakawa kwamba serikali ikawapa Waislamu nafasi iliyoombwa.

Itaendelea toleo lijalo Inshallah.

IJTIMAA YA ANSARULLAH - 2011

Sadr wa Majlis Ansarullah anapenda kuwakumbusha Ansarullah wote kwamba Ijtimaa ya Ansarullah itafanyika tarehe 10 - 11 Disemba 2011 katika eneo la Jumuiya Kitonga Dar es Salaam.

Ansarullah wote nchini wanaombwa kujindaakwaajiliyakuhudhuriaIjtimaahiyo.

Aidha Ansarullah wote wanakumbushwa kuhakikisha kwamba wanatoa michango yao ya Ijtimaa haraka iwezekanavyo kwani muda uliobaki ni mdogo.
Kiwango cha mchango ni angalau Tsh. 5,000/- (elfu tano kwa kila mtu)

Majlis Ansarullah Ahmadiyya - Tanzania

Tanzania yazidi kupoteza hazina zake

Na Mahmood Hamsin Mubiru

Kifo cha hivi karibuni, cha Mwinyihatibu Mohamedi Amir asadi katika biladi zetu, mwepesi wa kufutu hoja na bingwa mtemedeni wa lugha ya Kiswahili, kina makali kuwili mithili ya panga. Kwanza ni kupotelewa na simba wa uswahilini, mjuzi wa ndaro na ndarire za mashairi ya Kiswahili. Pili ni aibu kubwa kwa taifa hili ya kwamba kifo cha mtumishi huyu wa lugha ya Kiswahili kimepita hivi hivi bila habari zake kupewa thamani angalau ya thumni! Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.

Ni msiba mkubwa kwa taifa lisilojali watu waliojali na kulitumikia kwa uaminifu mkubwa. Mwinyihatibu ni miongoni mwa washairi wa mwanzo kabisa kueleza na kufafanua juu ya mapambano yetu kwa njia ya utenzi. Utenzi wake wa "Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika" ni lulu ya ushairi katika Tanzania. Utenzi huu ulihariri wa na kuwekewa shime na Sheikh Kaluta Amri Abedi. Kwa njia ya tenzi ametuachia harakati zetu za kujikomboa katika sanaa ya ushairi. Kwake Mwinyihatibu mashairi yalikuwa ni wajibu wa kuamsha waliolala ili sote tuweze kuvuta pamoja chombo chetu. Ndiyo maana ukisoma mashairi yake katika 'malenga wa Mrima', 'malenga wa Mrima amerudi', 'Tungo zangu', 'Mapenzi ya Mungu' hutakosa kunasa katika mistari yake ya johari ambayo inahimiza tangamano, mapenzi, huruma na elimu.

Mwinyihatibu Mohamedi Amri aliyezaliwa huko Tanga, Tangoni mwaka 1920 alianza kupiga mbizi katika bahari ya ushairi mwaka 1957. Akiwa anafanya kazi bandarini Dar es salaam alitunga shairi 'Tungo zimo hatarini' ambalo lilimvutia sana Mhariri wa gazeti la Mapenzi ya Mungu wakati huo gazeti lilikuwa likihaririwa na Sheikh Kaluta Amri Abedi. Mhariri huyo hakuweza kuvumilia kwenye dawati la uhariri bali alifunga safari hadi bandarini na kuonana na Mwinyi Hatibu Mohamedi na kumpa hongera na shumbe na kumuhimiza aendelee kutunga. Ni mkutano huo uliojenga urafiki mkubwa baina ya washairi hawa wawili. Ingawaje Mwinyihatibu alimzidi umri Sheikh Kaluta aliyezaliwa mwaka 1924 hilo halikuwa tatizo katika usuhuba wao. Mwinyihatibu aliendelea kutunga mashairi yenye kina kirefu cha hekima na kuwapa furaha ya abadi wasomaji wa gazeti la Mapenzi ya Mungu.

Yalipozuka malumbano yaliyoanzishwa na Shaaban Robert alipoandika shairi 'Ndoa mbaya afadhali kuliko ujane mwema' lilitokea tufani kubwa katika bahari ya ushairi na wakawa hawasikilizani. Kambi mbili ziliibuka, moja ikiongozwa na Pallamlanzi Hassan ambaye hakuona umuhimu na ulazima wa kuoa na kwa upande mwingine uliongozwa na Shaaban Robert akiwa na askari wafuatao; Mwanaidi, Akilimali Snow White, Sheikh Kaluta Amri Abedi na Mwinyihatibu Mohamedi Amri. Ni dhahiri ya kwamba bahari ya ushairi haijawahi kuchafuka kama wakati huo. Mabingwa wa Dodoma walisimama kidete kumpinga Shaabani Robert na maneno ya kebehi na dharau yalitumika pande zote mbili.

Khamas Amani Hamisi Nyamaume alikwenda mbali sana katika maneno yake ya ufedhuli, akaamsha hisia kali za mtoto kindaki wa uswahilini Shaabani Robert naye akatoka na upanga mkali.

Nyamaume wa Dodoma wasema nazoazoa
Kauli hiyo si njema vigumu kukuokoa
Wajao kwangu huzama hushindwa maogeleo
Sitateta naye chawa silaha ikawa chuma.

Naye Mwinyihatibu hakufurahishwa na upepo huo ulivyokuwa unavuma. Hususan kumuhusu Mahmood Hamduni (Jitukali) ambaye alionekana kutokuwa na msimamo na hapo Mwinyihatibu alitunga moja ya mashairi yake bora.

Mwetu wamehimikiza, kwa safu na kwa tabaka
Nyoyo ziwangile giza, kila twika hujitwika
Jitukali hakusaza, ndumile kumithilika
Ndumakuwili si mwema, hujidhuru nafsiye.

Suluhisho la malumbano hayo lilipatikana na washairi wakasameheana na kuendelea na kazi yao ya kuelimisha taifa. Mwinyihatibu Mohamedi aliendelea na utunzi na kuguswa sana na harakati za ukombozi wa nchi hii. Hili lilimsukuma atunge utenzi kuhusu uhuru wa nchi hii. Ni utunzi unaohifadhi historia yetu. Una utimilifu wa fani na ni mchango adhimu katika Taarikh ya ushairi. Tizama anavyofanikiwa kuua ndege wawili kwa jiwe moja -Maudhui na fani.

Tanu ilitapakaa
Kwanguvu ikasambaa.Nchini ikatambaa.Shabihi mlangamia.

Mwalimu Julias Kambarage Nyerere Mshairi na mpenzi wa fani hii aliposikia tetesi kuwa Mwinyihatibu ametengeneza pilao ya kukata na shoka, alimuomba asimnyime walau makoko. Kabla kazi hiyo haijachapishwa, Mwinyihatibu alimpatia kazi hiyo Sheikh Kaluta Amri Abedi wakati huo Meya wa jiji la Dar es salaam ili aipitie. Sheikh aliipitia na akafurahishwa sana na kazi hiyo. Mipango ilifanywa na Mwinyihatibu alisafirishwa na idara ya utangazaji hadi Dar es salaam alipomkabidhi Mwalimu Julius K. Nyerere nakala ya utenzi huo wa Uhuru wa Tanganyika. Hivi leo ni miswada mingapi inaliwa na mchwa na wala serikali haina habari? Utalindaje na kuenzi Kiswahili bila kuendeleza ushairi? Inatisha kuona Mwinyihatibu Mohamedi anaondoka na wala bendera hazipeperushwi nusu mlingoti. Je tunafahamu alipozikwa? Hazina alizoziacha tukubali ziliwe mchwa? Taifa linaweza kuendelea vipi bila ya Waandishi wake maarufu kusikilizwa na kuenziwa? Je tusubiri kwenda kujifunza Kiswahili London na Washington? Ukweli ni kwamba kazi zao zinakwenda nchi za



Mwinyihatibu Mohamedi Amir

ughaibuni na sisi tunaangalia. Tutaamka lini?

Mwanafalsafa wa namna hii tunakubali apite bila hata jani kutetema? Tizama falsafa aliyotuachia. Kwa sanaa ya ushairi warika lake ni akina Pallamlanzi Hassan, Shaaban Robert, Mdanzi Hanasa, Mohamood Hamduni Jitukali, Sheikh Amri na Matias Mnyampara. Falsafa katika mashairi yake ilikuwa ya juu. Kwa mfano alilinganisha cheo na ulevi na akasema:

Ni ulevi wa kikao, uendapo ukakuvaa
Hunyanyasa wapitao, ndugu na zako jamaa
Humtambui mwemao, na ajae wamwambaa
Fungueni makatasi, muone pombe na cheo

Juu ya ndumakuwili, utamaduni uliostawi sana katika jamii yetu, Mwinyihatibu anatoa tahadhari . Tusimuamini mtu wa namna hii na wala tusimpe kigoda kukaa.

Mtu mwenye ndimi mbili, baadhi humwita nyoka
Neno lake si la kweli, sura alivyopotoka
Ahadize si kamili, hachumi ila mashaka
Ndumakuwili ni nyoka, kuwa athiri unasi.

Binadamu siku zote hawezi kujiona yeye mwenyewe, ila kwa kupitia wengine. Katu huwezi kujiona mwenyewe. Hayo ndiyo Kashiyasi anamueleza Brutasi katika mchezo wa Julius Kaisari. Kalamu ya Mwinyihatibu imetutahadharisha sana kwamba mtu huwezi kujiona mwenyewe;

Kijiba huyabongoa, au kidudu kopeni
Huwezi kujitetea, ila upate jirani
Hayo yakitolekea, jicho limo hatarini
Pekee halijioni, jicho ila kwa mwenziwe.

Mtumai cha nduguye ni kweli hufa masikini. Ni kweli Kingereza ligha ya kimataifa na maarufu, lakini lazima tukumbuke siyo lugha yetu. Titi la mama ni tamu alitukumbusha Shaaban Robert na jingine halishi hamu. Mwinyihatibu anatuambia tupende chetu, tukitumai cha ndugu tutakufa masikini. Na chetu ni Kiswahili;

Hizo lugha zenye kimo, zasemwa kumi na mbili
Na hii yetu imumo, kwa madaha na fi ili
Imewamba kama mimo, kiwambani tamthili
Mtumai cha nduguye, hufa hali masikini.

Kupapatikia mambo ya kupita ni ujuha na ulimbukeni, lazima kufahamu ya kupita na ya kudumu. Si vizuri kutoa heshima kubwa sana kwa nanasi, kwani ni tunda la msimu. Usidharau ulichonacho, usiache mbachao kwa msala upitao. Nae Mwinyihatibu anasisitiza hilo;

Hayo mambo yapitayo, kama vuli na masika
Mtu hujigambi nayo, ada akaikeuka
Twaeni niyasemayo, waja walio hurika
Waacha wako mkeka, kwa zulia lipitalo.

Tatizo linalotukabili hivi leo, ni watu kusema wasiyoyatenda, wanapotuambia tufunge mikanda wao hawawezi kwa sababu ya vitambi vikubwa walivyo navyo. Wanaposema tutumie bajaji kwa mama wajawazito, wake zao wanakwenda kuzalia Washington au London. Hili ni tatizo kubwa sana katika Afrika. Maneno hayaendi sawa na vitendo. Mwinyihatibu Mohamedi anatuonya juu ya mwenendo huu;

Maneno yako matupu, pasi wewe kuanziliza
Shundia tumbo kwa kapu, na mengine kusaaza
Kamawe si chapuchapu, wanyuma kuyapuuza
Mja neno huigiza, si neno ila vitendo.

Hiyo ni sauti ya Mwinyihatibu. Ni dhahiri amefariki kwani kila nafsi itaonja mauti isipokuwa ameacha hazina kubwa. Ni wajibu wetu kukusanya kazi za Malenga na tusiache hata neno moja kwani kila neno lake limejaa wema. Na juu ya neno jema - Sheikh Kaluta Amri Abedi anatushauri;

Neno jema haliozi,
halifi halikauki
Kulipinza utahizi,
uvie kimo na maki
Udumae uwe bazi,
watu wasikushituki

MSIBA

1 Huzuni kabiri ajabu, roho zinaweweseka
Ametawafu muhibu, mtunzi wa kusifika
Amir Mwinyihatibu, Mohamedi katutoka
Kuanguka wetu mti, kivuli tupate wapi?

2 Ametutoka sahibu, wa hududi na mipaka
Kila neno na sababu, shufu alivyoandika!
Tungo zake ni zabibu, wala na kuburudika
Mto wetu kukauka, wapi tutapata maji?

3 Kwa methali na majibu, ni nani wa kumfika?
Wa kumfika Habibu, beti alivyoziweka
Hae! Hino ni sababu, shuara kuporomoka
Wa kujenga sasa nani, nyumba iliyoanguka?

4 Tupe mwingine wahabu, mahiri wa kukandika
Tupe mithili dhahabu, penye giza kung'arika
Tupe atayetutibu, ndwele zinapotushika
Kila ugonjwa na dawa, Rabbi tupatie dawa

5 Tamati kadi hesabu, malenga akishafika
Aweze yote kujibu, pasina kubabaika
Ili akwepe adhabu, iletayo patashika
Iwe hisaban yasira, mjao twamuombea

Mahmood Hamsin Mubiru (Wamamba)

Falsafa ya Masharti ya Baiat

Kutoka uk. 12

Islam kutokana na hali zao za kifasiki. Na wasiwe kama wale Madaruweshi walioghafilika na wale watu waliojitenga kabisa na dunia wasio na habari yoyote juu ya mahitajio ya Kiislamu na wasio na huruma yoyote kwa ndugu zao na hawana ari yoyote ya kuwanufaisha wanadamu, bali wawe ni wenye kuwahurumia watu kiasi hiki kwamba wawe ni kimbilio la masikini, wawe mababa kwa ajili ya mayatima na wawe tayari kujitoa muhanga kama yule aliyehemewa na mapenzi katika kuuhudumia Uislamu, na wafanye juhudi yote kwa ajili ya jambo hili kwamba baraka zao za kawaida zienee duniani na chemchem takatifu ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu na huruma kwa waja wa Mwenyezi Mungu itoke katika kila moyo na kujumuika sehemu moja na kuonekana ikitiririka katika sura ya mto utiririkao.

"Mwenyezi Mungu Anataka kuanzisha kundi hili na kulipatia mafanikio kwa ajili ya kudhihirisha ujalali wake na kuonyesha Kudra yake ili Aeneze mapenzi ya Mungu, toba ya kweli, utakaso, wema wa kweli, amani, suluhu na huruma kwa binadamu duniani kote. Hivyo kundi hili litakuwa ni kundi lake makhsus Naye Mwenyewe Atawapa nguvu kwa roho Yake na Atawalinda na maisha machafu na Ataleta mabadiliko matakatifu katika maisha yao na kama vile Alivyoahidi katika bishara zake takatifu kwamba Atalikuza sana kundi hili na Atawaingiza maelfu ya wakweli ndani ya kundi hili na Mwenyewe Atalilea kundi hili na kulistawisha kiasi ya kwamba uwingi wao na baraka zao zitawastaajabisha watazamaji, na wataeneza nuru yao pande zote nne za dunia kama ile taa iliyowekwa mahali pa juu nao watakuwa kama mfano wa baraka za Kiislamu.

"Atawapa ushindi wa baraka za kila aina, wafuasi kamili wa Jumuiya hii, dhidi ya watu wa silsila zingine na daima hadi Kiama watapatikana watu miongoni mwao watakaopewa msaada na kukubalika. Mwenyezi Mungu huyu mwenye shani Ametaka hivi hivi, Yeye ni Mweza, Hufanya Atakacho. Kila nguvu na uwezo vi Kwake."

Alitoa maagizo ndani ya tangazo hili hili kwamba watu watakaofanya Baiat wawasili Ludhiana baada ya tarehe 20 March. (Majmuua Ishtihaaraat jal. 1 uk. 196 – 198).

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah.

Masihi a.s. ajibu maswali:

Sala ambazo hazikusaliwa:
Masihi Aliyeahidiwa (a.s) aliulizwa na mtu mmoja ambaye kwa mfululizo miezi sita alikuwa hakusali kama angeweza kulipia sala hizo ambazo hakusali. Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema hiyo haiwezekani na akasema sala ambazo hazikusaliwa katika siku zilizopita haitakiwi zisaliwe.

Kuheshimu Kaaba:
Masihi Aliyeahidiwa (a.s) aliulizwa kama mtu anaweza kunyoosha miguu kuelekea Kaaba. Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alisema; Hapana. Alisema kufanya hivyo ni kutoonyesha heshima kwa Kaaba. Muulizaji alisema lakini haikukatazwa katika hadithi au mahali popote pale. Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema hiyo ni hoja isiyo na uzito. Unafikiri alisema inaruhusiwa kusimama juu ya Kurani Tukufu? Kwa sababu tu haikutajwa katika Kurani Tukufu, kwa hiyo tufanye hivyo? Baadaye akasoma aya ya Kurani Tukufu isemayo; Yule ambaye anaheshimu alama za Mwenyezi Mungu anafanya hivyo kwa sababu ya ucha Mungu wake.

Kuwaombea waliokufa:
Masihi Aliyeahidiwa (as) aliulizwa ni maombi yepi kwa lugha ya Kiarabu yanatakiwa yaombwe kwa aliyefariki? Alisema zote hizo ni desturi na kanuni. Nyinyi muombeni Mwenyezi Mungu katika lugha zenu na maombi yawe kwa aliyekufa.

Je watu wawili wanaweza kusali Ijumaa?
Masihi Aliyeahidiwa aliulizwa; Je inaruhusiwa ikiwa wapo Waahmadiyya wawili mahala wanaweza kusali sala ya Ijumaa? Masihi Aliyeahidiwa (as) alimgeukia Maulvi Muhammad Ahsan na kutaka atoe maelezo. Yeye alisema sala ya Ijumaa inaweza kusaliwa na watu wawili. Halafu Masihi aliyeahidiwa (as) akasema ndiyo inabidi wasali sala ya Ijumaa. Ingawaje Fiq'hi ya Islam inasema wawepo watu wapatao watatu (3) Lakini mimi naona ya kwamba kama mtu yupo peke yake (Mwanaume) amwambie mke wake wasimame wawili na wasali sala ya Ijumaa (Al-Hakam, March 10, 1905).

Sera ya Jamaat kuhusu matumizi ya mtandao Jamii "Facebook"

Kufuatia hutuba aliyoitoa Khalifatul Masih V huko Ujerumani alipokuwa akifunga mkutano wa mwaka wa nchi hiyo (Jalsa Salana) tarehe 26/06/2011, Huzur(a. t.b.a) alizungumzia mambo mbalimbali. Miongoni mwa mambo hayo ni matumizi ya aina mbalimbali ya mitandao ya 'kompyuta' ambapo Amirul Muuminiin alielezea faida na hasara inayopatikana katika kutumia mitandao hiyo na hasa mtandao wa jamii ujulikanao kwa jina la "Facebook".

Kutokana na uzito wa hotuba hiyo Kamati maalum ya MTA ilitoa mapendekezo ya Sera ya Jamaat Ahmadiyya juu ya matumizi ya mtandao huo. Mapendekezo hayo yalipelekwa mbele ya Khalifa Mtukufu (atba) ambae aliyaidhinisha. Napenda kuanisha sera hiyo hapa chini ili kila Mwanajumuiya afahamu msimamo wa Jamaat juu ya matumizi sahihi ya mitandao hii, hasa mtandao wa Facebook, kama ilivyotolewa na Markaz ya London kupitia Idara ya malezi katika Tanzim ya Khuddamul ahmadiya;

1. Mwanajumuiya yeyote haruhusiwi kuanzisha kurasa za "Facebook" kwa niaba ya Jumuiya ya waislam wa ahmadiyya. Kurasa zote zilizofunguliwa na watu binafsi zikiwakilisha, " ahmadiyya", au "Mirza Ghulam ahmad Qadian (a.s) ", au "Masih aliyeahiwa (a.s)" au "Mirza Masroor ahmad "au "Khalifatul Masih" nk Lazima zifungwe mara moja.
2. Mtandao pekee ulio rasmi unaowakilisha Jumuiya ya waislam wa ahmdiyya ni ule unaopitia kwenye tovuti ya alislam kwa anuani ya http://www.facebook.com/Ahmadiyya Muslim
3. Imekatazwa tabia ya Kufungua na kutumia kurasa au akaunti binafsi ya "Facebook" kwa wanajumuiya .(Kumb: hutuba ya kufunga Jalsa Salana ya Ujerumani iliyotolewa na Hadhrat Khalifatul Masih V, tarehe 26 Juni 2011).
4. Kama una swali lolote, muandikie mwenyekiti wa alislam kupitia anuani hiiya barua pepe; nasim. rehmatullah@ahmadiyya.

Haya ni baadhi ya maswali ambayo wengi wamekuwa wakiuliza mara kwa mara pamoja na majibu yake;

Swali. Kama wanajumuiya hawaruhusiwi, kuwa au kutumia Facebook, mbona jumuiya inaendelea kuwa na Facebook kwenye mitandao ya Internet?

Jibu: kuna sababu nyingi za kuanzishwa au kuwepo kwa mtandao huu wa Jumuiya (1) kuwa ni mtandao rasmi wa Jumuiya ya ahmadiyya dhidi ya wasio Wahmadiyya, na kujibu shutuma zao. (2) Kutoa mafunzo sahihi ya dini tukufu ya Islam. Hata hivyo haihitajiki akaunti ya Facebook kuupata au kuufikia ukurasa wa Jamaat Ahmadiyya, yeyote anaweza kuufikia ukurasa huo na kupata mambo mapya kabisa kwa anuani ya http://www.facebook.com/AhmadiyyaMuslim

Swali; kukatazwa huku kwa wanajumuiya kutumia mtandao wa Facebook, kunafanya pia tusiruhusiwe kutumia mitandao mengine ya kijamii?

Jibu: Inategemea, Facebook msingi wake mkubwa ni kuondoa usiri, kuwekana wazi na kutoa taarifa za ndani za muhusika. Kwa maana hiyo, kukatazwa huku kutakwenda sambamba na aina zote za mitandao ya aina hii, Kama vile MySpace, hi5, Google nk. Hata hivyo tangazo hili haliingii katika mitandao ya kijamii yenye mitazamo tofauti kama vile Twitter au LinkedIn. Kimsingi kuwa muadilifu kuamua au uliza.

Zaidi ya hayo, wanajumuiya wanatakiwa kuwa makini na kuchukua tahadhari kubwa katika matumizi ya mitandao hii isiyokatazwa ili kuhakikisha kwamba iko salama, inalindwa, haina muingiliano haswa kwenye habari za watu na haki zake zimehifadhiwa. Wazazi wametakiwa hasa kuwaelimisha watoto wao juu ya matumizi sahihi ya mitandao hii.

Swali: Je!, Kukatazwa huku kwa wanajumuiya kutumia mtandao huu wa Facebook, kunahusisha pia na mitandao ya facebook ya kibiashara au kielimu?

Jibu: Hapana, uundwaji na malengo ya mitandao ya facebook ya kibiashara na kielimu ni tofauti na ya ile ya mtu binafsi, kwa hiyo haiingii kwenye ile iliyokatazwa, inashauriwa kutumia kwa tahadhari.

Swali: Je naweza kuendelea kutumia anuani yangu ya Facebook ikiwa nitaitumia kwa uangalifu?

Jibu: Kwa ujumla kuna ubaya zaidi katika mitandao kama ya facebook, na inaleta uwezekano mkubwa wa matumizi mabaya au udhalilishaji. Kwa hiyo kukatazwa huku, haswa kunalenga kuwalinda wanajumuiya kwa ujumla wake.

Tujihadhari na Samaki toka Japani

Na Yasin Shoo, Dar es Salaam

Serikali imezuia kuuzwa kwa samaki walioagizwa kutoka Japan na kuamuru uchunguzi ufanyike ili kubaini kama Samaki hao kama wameathiriwa na mionzi ya Nyuklia.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Dk. Haji Mponda, Baada ya kukagua maghala ya kuhifadhia Samaki ya Kampuni ya Alpha Crist iliyopo Kipawa, Jijini Dar es Salaam, Kampuni hiyo inadaiwa kuingiza nchini kontena tano zenye uzito wa tani 25 kila moja za Samaki aina ya Kamongo na kibua wiki tatu zilizopita kutoka nchini Japan na kuzusha hofu ya kuwepo kwa mionzi hiyo hatari.

Dk. Mponda alisema Serikali imefanikiwa kukusanya sehemu kubwa ya Samaki ambao walikuwa wameshasambazwa nchini kwa ajili ya kuuzwa na kuwaweka katika uangalizi maalum.

Alisema wakati shehena hiyo imezuiwa, Hatua mbalimbali zinafanyika ikiwa pamoja na kufanya uchunguzi wa kimaabara kuona samaki hao wapo salama kwa walaji. "Serikali inawasiwasi na Samaki hawa waliotoka Japan, Tumeamua kuwazuia wasiuzwe na shehena zote zilizopelekwa mikoani tumezirudisha " alisema Dk. Mponda.

Dk. Mponda alisema waataalamu toka Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) wameanza kuangalia Sampuli ya Samaki hao kabla ya Serikali kutoa tamko rasmi.

Naye Mkurugenzi wa Kampuni iliyoingiza nchini Samaki hao Bwana Ganesh Vedgir alisema anaamini Samaki hao wapo Salam kwa Sababu wamehakikiwa na Idara zote za kuangalia usalama wa Chakula za hapa nchini na nchini Japan, Alisema kabla ya kuingizwa nchini alipeleka sampuli TFDA na kukubaliwa samaki hao ni salama na wanafaa kuliwa na binaadamu.

Lakini naye Waziri Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi Dk. David Mathayo akitoa taarifa bungeni alikiri kuwepo zaidi ya tani 123,600 za Samaki hao ziliingizwa nchini na tayari wapo sokoni. Dk. Mathayo Samaki hao waliingizwa nchini katika mazingira yaliyojaa utata licha ya vibalin vyote kutolewa na Serikali, Kwamba Serikali iliamua kufuatilia kwa utaribu mzima wa uingizaji wa Samaki hao.

Kibali cha tume ya Atomic kilipatikana Julai 8, Cha uvuvi kilipatikana Julai 8, na kibali cha TFDA Namba 11/F/IER/0896 kilipatikana Julai 23 mwaka huu ambayo ndio siku shehena hiyo iliingizwa nchini na Kesho yake samaki hao wakaanza kusambazwa.

Baada ya ya kuzuia wasiuzwe wala kusambazwa mpaka hapo serikali itakapojihakikishia usalama kwa walaji wa samaki hai kwani Waziri Dk. Mathayo alisema sampuli za samaki hao zimepelekwa nchini Kenya na Afrika Kusini kwa ajili ya uchunguzi zaidi ili kubaini kemikali zilizomo ndani yake.

Tanzania ina ukubwa wa bahari ya Hindi yenye urefu wa kilomita 1424, upana kilomita za mraba 64,000 na samaki aina ya kibua walioingizwa kutoka Japan wanapatikana kwa wingi katika eneo hili. Tunajiuliza kwamba hivi tuna haja ya kuingiza samaki toka Japan?

Apata embe

Kutoka uk. 12

huku akitetemeka na kwa huzuni kubwa alimshangaa kiongozi wa dini akidiriki kusema uongo na huku ameshika kitabu kitakatifu. Rohoni alisema kama viongozi wetu wa dini wako hivi basi bila shaka ni afadhali kuwa Mkristo. Hii ilimkumbusha pia hadithi ya Mtukufu Mtume (s.a.w) iliyosema ya kwamba Masheikh watakuwa watu wabaya sana chini ya ardhi. Muzaffar alisema ya kwamba aliielewa zaidi hadithi ya Mtume (s.a.w) mara baada ya yule Sheikh kutoa ushahidi wa uongo.

Maisha ya Muzaffar Ahmad yalikuwa magumu sana jela. Iliaminika ya kwamba unazidi kupata thawabu kadri unavyoendelea kuwatesa Ahmadiyya kwani wao ni makafiri na kuna haki ya kuwatesa. Kazi ngumu walipewa hao vijana wawili wa Kiahmadiyya. Wakati wakiendelea na mateso hayo hukumu ilipita ya kwamba ushahidi wa kutosha umepatikana na hivyo vijana hao wanasubiriwa tu kupangiwa siku ya kunyongwa.

Baadhi ya watuhumiwa wawili ambao waliwekwa tu kwa mtindo wa geresha walitolewa ndani na kubaki hawa Waahmadiyya wawili. Wakiendelea na maombi humo jela waliweza kuomba rufaa. Wakati wakisubiri matokeo ya rufaa yao kiongozi wa Jumuiyya ya Waislam Waahmadiyya duniani (wakati huo) Hadhrat Mirza Tahir Ahmad alimuandikia barua Muzaffar Ahmad ya kwamba amemuona katika mtaa mmoja wa London akimpatia zawadi ya maembe. Na alimueleza pia katika barua hiyo kwamba embe hizo alimpatia wakati wa msimu wa embe.

Miezi mitatu baadae njozi hiyo ya Huzur ilitimia neno kwa neno, na Bw. Muzaffar Ahmad alitolewa jela ilikuwa ni usiku wa manane na kupelekwa hadi kwenye Jamaat ya Lahore ambako mipango ilifanywa ya safari ya Bw. Muzaffar kwenda London. Na huko alipata bahati ya kupokewa na kiongozi wa Waaminio na kupewa zawadi ya embe.

Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya yaweka Historia mpya

Kutoka uk. 12

Jamaat ambao Majlis Amila yote inapigiwa, katika Tanzeem ni uchaguzi wa Qaid tu ndio unaofanyika na taarifa yake kutumwa kwa Sadr kwa idhini. Baada ya kikao cha Iringa mjini ambacho kilihudhuriwa na khuddam kutoka matawi ya Mkwawa, Mtwivila na Gangilonga, msafara wa Sadr ulipata chakula na mapumziko tayari kwa siku iliyofuata.

Safari ya kuelekea Mbeya ilianza ukipitia Jamaat za Kinegembasi na Songambele. Mwalimu Bashir Mrope wa Kinegembasi akiwa na Khuddam na Atfal kadhaa waliungana na msafara kuelekea Songambele kwa ajili ya kikao. Jamaat ya Songambele ambayo imo katika Wilaya ya Mufindi umbali wa takriban maili 15 toka barabara ya Mbeya ambapo tulikuta wenyeji wetu wakiwa chini ya Mwalimu Ahmad Msola na kufanya kikao ambacho kilihudhuriwa na Khuddam siyo tu wa Songambele pia walikuwepo khuddam kutoka Jamaat ya Mkangwe ambayo Bw, Naib Kivambe na Atfal watatu waliwakilisha.

Jamaat ya Songambele imefanya jitihada kubwa ya kujenga msikiti kwa nguvu zao wenyewe na kusaidiwa bati toka Makao Makuu. Sadr sahib alikabidhi mchango wa fedha katika kuwaunga mkono katika juhudi zao za kujitegemea kujenga msikiti huo.

Pia Sadr alionyeshwa kisima kilichochimbwa na wanajamaat na kuwa mkombozi wa shida ya maji katika kijiji hicho chenye utajiri mkubwa mazao ya mahindi na ardhi yenye rutuba. Sadr aliwapongeza kwa kazi nzuri ya kuhudumia watu na kutoa huduma kwa wanaotuzunguka.

Baada ya kikao cha Songambele safari ya Mbeya ilianza na kufika majira ya Magharibi na tulikuta Khuddam wakitusubiri kwa hamu kubwa wakiongozwa na Qaid wa tawi la Mbeya Bw, Abdallah Ahmad Nauja. Ansarullah wakiongozwa na Dr. Mwanga pia alikuwepo muda wote wa kikao.

Baada ya kupokea taarifa kutoka kwa Qaid wa tawi, Sadr alianza kikao kwa kuongoza maombi ya kimya baadaye kiapo cha Khuddam kilifuatia. Sadr aliwashukuru khuddam kwa uvumilivu wao wa kutusubiri bila ya kuchoka na pia aliwashukuru ansarullah tuliokuwa nao muda wote na kuwaelezea kuwa nafasi yao ya uzazi na ulezi wana wajibu wa kujua vijana wao tunayoyafanya kwani ni washauri wetu katika mambo mengi ya khuddam.

Sadr sahib baada ya kumtaka Mu'utamad kuweka mbele ajenda za kikao ambazo zilipitiwa na kuelezwa kikamilifu kuanzia ile Ijtmaa na shura, maendeleo ya jengo la ofisi zetu za Tanzeem linalojengwa huko Kitonga



Picha ya pamoja kati ya Wanajamaat wa matawi ya Makka na Madina Kilangalanga Songea na uongozi wa Khuddamul Ahmadiyya taifa wakati ulipotembelea tawini hapo.

mjini Dar es Salaam na pia hali ya uongozi wa Tanzeem katika tawi la Mbeya ambapo alimtaka Qaid wa tawi aunde majlis Amila na amtumie Sadr kwa idhini. Kikao kilifungwa kwa maombi na kupata chakula cha usiku kwa Khuddam mwenzetu, Mbashiri wa Mkoa wa Mbeya Sheikh Basharat-ur-Rehman Butt na kupata malazi nyumbani kwa Muhtamim Mal Bw, Issa Mwakitalima.

Siku iliyofuata baada ya kupata chai kwa chapati za kipwani nyumbani kwa Mwalimu Makarani Hamza, ilikuwa ni zamu ya Jamaat za Busale na Ibonde na tuliwachukua khuddam wa Busale na kikao tulikifanya Ibonde ambayo inapatikana katika Wilaya ya Kyela. Jamaat imefika mbali kwenye kupanuka kwake kwani ilituchukua mwendo wa kwa mguu wa dakika zaidi thelathini na kuvuka mto mdogo ili kuwafuata khuddam wa huko.

Sadr sahib aliongoza mwendo huo na alikuwa na hamu ya kuwaona khuddam na hatimaye tulifika Ibonde na kufanya kikao na kuanza kuwapatia taarifa ya ijtmaa na shura, kuwapatia taarifa ya ujenzi wa ofisi zetu na kuunda safu ya uongozi katika matawi ya Ibonde na Busale ambayo haikuwepo.

Sadr alipata nafasi ya kumtembelea Katibu wa tawi la Ibonde ambaye alikuwa ni mgonjwa ambapo alimpa pole na baada ya kushauriwa alimkabidhi fedha kidogo ili aweze kwenda hospitali na Daktari aliyekuwepo kwenye msafara wa Sadr alimpa vidonge kama huduma ya kwanza.

Sadr sahib aliongoza msafara wa kurudi Mbeye Mjini na moja kwa moja kuelekea Songwe nyumbani kwa Mzee wetu Dr. Iddi Mwanga na kufanya nae mazungumzo na aliandaa chakula cha usiku kwa msafara na alitutembeza nyumbani kwake kujionea maisha ya Ansarullah huyu ambaye ni daktari mstaafu anayeonekana kupenda sana kilimo. Aidha Dr. Mwanga alituasa kama khuddam tukipata nafasi ya kazi basi tusisahau kilimo na kutupa historia fupi iliyomfanya yeye kutoka Muhimbili na kuhamia Mbeya ni kwa sababu ya hali ngumu ya uchumi na kupatikana kwa shida kwa mahitaji muhimu mwanzoni mwa miaka ya themanini, miaka ambayo Serikali iliwataka Watanzania kufunga mikanda. Msafara ulirejea Mbeya kwa mapumziko.

Siku iliyofuata msafara ulianza safari ndefu ya kuelekea Mkoa wa Ruvuma na hatimaye tulifika Jamaat ya Mkongotema ambapo Mwalimu Kaisi aliwaandaa Khuddam na Atfal waliupokea msafara wa Sadr kwa shangwe na bashasha isiyo kifani na kabla ya kuanza kikao Mwalimu alituongoza kwenda kuwaona viongozi wa Serikali na hii ni kutokana na uhusiano mzuri uliokuwepo kati ya Jamaat na Serikali wa kata ya Mkongotema. Sadr alipata nafasi ya kuonana na Mtendaji wa Kata na Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji cha Mkongotema na kueleza furaha yao ya kupata ugeni na Mwenyekiti alimuelezea Mwalimu Kaisi kuwa ni mshauri wake mkubwa kwenye masuala ya uongozi katika eneo lake na ilifikia hatua ya kupendekeza kuwa huyu bwana asihamishwe hapa wazo ambalo Sadr alisema haliwezekani kwa taratibu za Jamaat.

Sadr sahib baada ya kukaribishwa kwa shairi zuri aliongoza maombi ya kimya na kufuatia kwa kiapo cha khuddam na moja kwa moja alianza kueleza madhumini ya safari yake. Baada ya kuutambulisha msafara alioongozana nao na kumtaka katibu kueleza ajenda za kikao, alieleza matarajio yake kuwa wana tanzeem wa Mkongotema watapata mkao mpya juu ya haya ambayo tumeyaeleza. Sadr alimuomba Mwalimu asaidie apatikane kiongozi na kuunda safu ya uongozi wa tanzeem na akamuomba aendelee kusaidia kuwalelea khuddam ambao bado ni wachanga katika kuelewa shughuli za tanzeem.

Kikao kilifungwa kwa maombi ya kimya ikafuatia dhifa ya kukata na shoka. Baada ya hapo msafara uliendelea na safari kuelekea Songea mjini na hatimaye tulifika salama. Alhamdullilahi. Baada ya mapumziko mafupi tulipata chakula cha usiku ambacho utamu wake itachukua muda mrefu kukisahau nyumbani kwa Mbashiri wa Mkoa wa Ruvuma Sheikh Abid Mahmood Bhati. Hatimaye akatupatia nyumba ya wageni ndani ya viunga vya msikiti na tukapata malazi.

Asubuhi yake ilikuwa ni zamu ya kufanya kikao katika Wilaya ya Mbinga na msafara ulielekea Mbinga na tukamkuta Mwalimu wetu Athumani Mgunya na Rais wa tawi la Mbinga wakitusubiri kutupokea, baada ya kupata chai ya asubuhi, Sadr alikaribishwa kuanza kikao chake na khuddam na Atfal waliokuwa makini walifikishiwa madhumuni ya safari.

Sadr Khuddamul Ahmadiyya alimtaka katibu aweke mbele ajenda za kikao na baada ya kikao aliwauliza kama tuliyoyafikisha yanatekelezeka na wote kwa pamoja walionyesha jazba na kuahidi kubadilika kwa mkao wao ambao walikiri kuwa ulikuwa si mzuri kwa upande wa khuddam. Sadr alipata faraja kusikia hilo na faraja kubwa zaidi ni ile ya kupata habari kuwa Jamaat ya Mbinga ndiyo inayoongoza kwa michango katika Mkoa Ruvuma.

Sadr sahib aliwataka changamoto hiyo pia ielekezwe kwa Tanzeem kwani humo ndimo kwenye siri ya mafanikio na kumuomba Mwalimu atusaidie kusimamia uchaguzi katika matawi ya Mbinga na Mbangamao.

Kikao kilifungwa kwa maombi ya kimya yaliyoongozwa na Mwalimu Athumani Mgunya na safari ya kurudi Songea ilianza.

Kikao cha Jamaat ya Songea kilianza muda mfupi baada ya sala ya Ijumaa na khuddam waliokuwa makini walikuwa tayari na mara baada ya Usomaji wa Qur'an Tukufu iliyosomwa na Ayub Mtekateka Sadr Sahib aliwaongoza Khuddam kwenye kiapo cha Khuddam.

Baada ya katibu wa kikao kuweka mbele ajenda aliwaomba khuddam wawe makini na wasikivu ili wajue jukumu lao la kufanya kazi za Jamaat. Sadr aliwakumbusha khuddam jukumu letu la kufanya tabligh, waqar amal na mambo mengine mengine na kwamba sisi ndio chachu ya maendeleo ya Jamaat. Mahala ambapo Jamaat imejisahau basi ni kazi yetu kuikumbusha Jamaat kwa kufanya kazi husika ili shughuli za Jamaat zisimame.

Sadr aliwataka Khuddam wa Songea wachangamke kwani Songea ni Jamaat kongwe na kuzubaa kwao kunadumaza maendeleo ya Jamaat. Watu wajitolee muda wao na wasione kufanya kazi za jamaat ni kupoteza muda, bali kuna fadhila kubwa sana na hivyo ni wajibu na haki yetu kama vijana tupate fadhila hizo.

Kikao kilifungwa kwa maombi na baadaye tulipata chakula cha mchana toka kwa mwalimu wetu makini Bw. Abubakari Maswa. Jioni tulipata kumtembelea mama mzazi wa dereva wetu katika msafara Bw. Chikulupi Kawinga na tukapata chakula cha usiku huko kwa mama. Jazakumullah.

Asubuhi yake msafara ulianza safari ya kwenda Kilangalanga na tulifika huko na kukuta wenyeji wetu wamejiandaa vilivyo. Khuddam na Ansarullah wote kwa pamoja walionyesha ushirikiano wa hali ya juu na kwa hakika tukapata chai ya kupendeza iliyotupa nguvu na ari na ikaondoa uchovu wa safari.

Tangazo la spika lilitumika kuwatangazia Khuddam wote wa Jamaat za Makka na Madina na mara moja walikusanyika na pia wanafunzi wa Sekondari wapatao 13 waliombewa ruhusa na Qaid wao na kikao kikaanza.

Sadr aliongoza kiapo cha khuddam na alimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuona Jamaat inayoonekana kuwa imara na angependa kuona Khuddam wanakuwa imara zaidi.

Sadr alifikisha maudhui ya safari na kuwaambia khuddam wanapotaka kufanya jambo lao basi ni lazima wahakikishe mipango yao haikinzani na ya jamaat na kwa kuwa viongozi wenyewe ni walewale basi ni vyema mashauriano. Ikitokea Jamaat imepanga mpango wake basi ule wa Tanzim lazima uhairishwe ili kuupisha mpango wa Jamaat kwani ndio wenye nafasi sawa na nidhamu yetu ndani ya Jamaat.

Baada ya kufikishiwa taarifa ya Ijtmaa na shura, maendeleo ya jengo, khuddam waliombwa kukaa sawa kwani kuna kazi kubwa mbele yetu inayohitaji mchango wetu.

Sadr alimuomba Mzee Mbawala kuongoza maombi ya kufunga kikao na kupata chakula cha mchana kilichoandaliwa kwa ajili yetu ambacho pia kiliweza kutupa nguvu mpya kwa ajili safari ya kuelekea Lusewa.

Safari ya Lusewa ilianza na tuliingia Lusewa tukawakuta ndugu zetu wakiwa hawaamini kama kweli Sadr wa Majlis Khuddam anaweza kufika Lusewa ambapo ni karibu mno na nchi ya Msumbiji. Wakielezea furaha yao walisema wanajiona kama wamezaliwa upya katika imani hii kwa Masihi Aliyeahidiwa.

Mwalimu Maliki Sandali aliwapanga vijana wakiongozwa na Katibu wa Jamaat wa tawi la Lusewa, khuddam mahiri Bwana Rajabu Sangana wakishirikiana na Rais wa Jamaat walifanya maandalizi kabambe.

Itaendelea toleo lijalo Inshallah.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

Mapenzi ya Mungu

Sha'ban 1432 AH | Julai 2011 | Wafa 1390 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Hurairah r.a. aliyesema ya kwamba Nabii s.a.w. alisema: Asiyeachana na kuongopa na kudanganya, Mwenyezi Mungu Hana haja ya kwamba yeye mtu huyo aache chakula chake na kunywa kwake. (***Bukhari***)

Falsafa ya kina ya Masharti ya Baiat

[HOTUBA YA HADHRAT KHALIFATUL MASIH V ATBA]

Hata kabla ya Hadhrat Masih Maud a.s kuanza kuchukua baiat baadhi ya watu wenye asili ya wema na watawa walioionea uchungu Islam wakahisi kwamba kama kuna mtu yeyote wakati huu mwenye uchungu wa kweli juu ya Islam awezaye kuliokoa jahazi hili la Kiislamu lililoelekea kuzama, basi huyo si mwingine bali Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. wa Qadian na huyu huyu ndiye Masihi na Mahdi pia. Hivyo watu wakawa wanamuomba kwamba tafadhali chukua Baiat. Lakini Huzur alikuwa daima akitoa jibu hili hili;

"Mimi bado sijaamrishwa.

Hatimae safari moja alimwandikia waziwazi Bwana Maulvi Abdul Qaadir kupitia kwa Bwana Mir Abaasi Ali akisema hivi:-

"Asili yangu imetawaliwa na Tauhid (Umoja wa Mwenyezi Mungu) na kuyakabidhi masuala yote kwa Mwenyezi Mungu, na kwa kuwa hadi sasa Mwenyezi Mungu hajanipasha habari yoyote kuhusiana na Baiat, hivyo haijuzu kuchukua hatua katika hali ya kujikalifisha.

'Huenda Mwenyezi Mungu baada ya hayo Akadhihirisha jambo.'

"Basi Maulawi Sahib ajitahidi kukuza undugu wa kidini. Na ajishughulishe katika kuustawisha mmea huu kwa chemchemi safi ya ikhlasi (uaminifu) na upendo. Basi njia hii hii ndiyo itakayonufaisha sana, INSHAALLAH."

(Hayat – e - Ahmad Jalada la Pili Nambari 2 Uk. 12 – 13)

Mwishowe baada ya miaka 6 au 7 katika miezi mitatu ya mwanzo wa mwaka wa 1888, alipokea amri toka kwa Mwenyezi Mungu ya kuchukua Baiat. Hukumu hii ya Mwenyezi Mungu ilifunuliwa kwa maneno haya;

(Tangazo la tarehe 1 December, 1888).

Ufungapo nia basi umtegemee Mwenyezi Mungu. Na utengeneze safina mbele ya macho yetu kulingana na ufunuo wetu. Wale watu watakaofanya baiat kwa mkono wako basi mkono wa Mwenyezi Mungu utakuwa juu ya mikono yao.

Tabia ya Hadhrat Masih Maud a.s ilikuwa inakirihika na jambo hili kwamba mtu wa kila aina aingie tu katika Silsila hii ya Baiat. Na moyo wake ulitaka hivi kwamba ndani ya hii Silsila iliyobarikiwa waingie tu wale watu waliobarikiwa wenye matini ya uaminifu ndani ya asili yao na wasio walegevu.

Hii ndio sababu iliyomfanya aisubiri fursa i t a k a y o w a p a m b a n u a waaminifu na wanafiki. Basi Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa Hekima na Rehema Yake isiyo na kifani, Akaifanya fursa hiyo itokee mnamo mwezi wa Novemba wa mwaka huo huo wa 1888 kutokana na kifo cha Bashir wa kwanza. (Huyu alikuwa ni mtoto wa kiume wa Hadhrat Masih Maud a.s).

Makelele ya upinzani dhidi yake yakavuma nchini kote na watu wenye imani dhaifu wakajenga dhana mbaya na kujitenga naye. Hivyo kwa mtazamo wake hii ikawa ndio fursa inayofaa kuanzisha silsila hii yenye baraka. Naye akatangaza wazi wazi tangazo la Baiat mnamo tarehe 1 Desemba 1888. Hadhrat Masih ul Maud pia akaagiza kwamba watu wahudhurie kwenye kufanya Baiat baada ya kufanya maombi ya Istikhara sawa na sunna ya Mtume s.a.w.

(imetoka kwenye Ishtihar Takmil e Tabligh 12 Januari 1889). Yaani kwanza wafanye maombi halafu wafanye Istikhara ndipo wafanye Baiat. Baada ya tangazo hili Hadhrat Masihul Maud a.s. akaelekea Ludhiana akitokea Qadian na akafikia katika nyumba ya Hadhrat Sufi Ahmad Jan iliyopo kwenye mtaa wa Jadid. (Hayate Ahmad jal.3 sehemu ya 1 uk 15).

Huko Ludhiana Masihi Aliyeahidiwa a.s. akachapisha tangazo lingine mnamo tarehe 4 March, 1889 akieleza shabaha na makusudio ya Baiat kwa kusema:

"Mfumo huu wa Baiat umeanzishwa tu kwa ajili ya kuwakusanya wacha Mungu katika Jumuiya ili kundi kubwa la wacha Mungu litoe athari yake njema duniani. Umoja wao uwe chimbuko la baraka na taadhima na matokeo mema kwa ajili ya Islam. Na kutokana na kuafikiana kwao juu ya Kalima moja yenye baraka waweze kutumika kwa haraka katika kutoa hudumu tukufu za Kiislamu na wasiwe Waislamu wavivu na wabakhili wasiokuwa na faida yoyote. Wala wasiwe kama wale watu wasiokuwa na thamani walioleta madhara makubwa kwa Islam kutokana na kutoafikiana kwao na kufarakana na wakatia doa kwenye uso mzuri wa

Endelea uk. 9

Apata embe badala ya Kifo

Na Mahmood Hamsin Mubiru

Mahakama. Mawakili. Na Wanasheria waliobobea. Korti ya Kijeshi. Vyombo vyote hivi kwa sauti moja vilikwishatangaza kuwa kama ilivyokuwa haiwezekani kwa ngamia kupita katika tundu la sindano hivyo hivyo Bw. Muzaffar Ahmad, Mhandisi wa umeme aliyezaliwa mwaka 1958 Sindh -Pakistan na kuhitimu kutoka chuo kikuu cha Mehren asingeweza kupona katika kesi kubwa ya uhaini iliyokuwa inamkabili. Lakini kama alivyosema Shaaban Robert kuna mkono wa siri unaofanya kazi siku zote. Ni dhahiri hakuna msiba unaompata binadamu hadi kibali kimetoka kwa Aliyetuumba.

Mwaka 1985 Zia-ul-Haq kiongozi wa kijeshi wa Pakistani alitibua historia nzima ya nchi hiyo ambayo ilianzishwa mwaka 1947 kwa kutangaza sheria ya kuwaondoa Waahmadiyya katika Islam. Hatuna mfano mwingine wa kipuuzi namna hii katika Taarikh ya Kiislam. Waahmadiyya hawakuruhusiwa kusoma Kalima. Kutoa Adhana. Mahali pao pa ibada kuitwa Msikiti. Kutoa Assalaam Alaikum. Ilikuwa ni wakati wa giza na fujo nyingi na uhasama wa hali ya juu dhidi ya Waahmadiyya. Serikali yenye kazi ya kulinda raia na mali zao ikashiriki kikamilifu katika kuwakandamiza Waahmadiyya ambayo Historia nzima ya Pakistani inaonyesha ndio walioshiriki katika kuleta uhuru wa taifa hilo la Pakistani.

Fujo nyingi na uhasama wa hali ya juu dhidi ya Waahmadiyya viliongezeka siku hadi siku, nyumba za Waahmadiyya zikichomwa moto, wakifunguliwa mashtaka ya uongo na kweli na kila singizio kwa Waahmadiyya lilikubaliwa bila kuhoji. Katika msururu huu wa masingizio hayo Msikiti mmoja unaojulikana kama Najum-ul-Haq ulishambuliwa kwa bomu na watu wasiojulikana. Bila aibu yoyote viongozi wa Msikiti huo walidai ya kwamba walioshambulia Msikiti huo ni Muzaffar Ahmad na kijana mmoja wa Kiahmadiyya.

Wanajumuiyya hao wawili walikamatwa na kuwekwa ndani. Kesi ilinguruma na ushahidi ukatafutwa huku na huku ili kuwaweka hatiani. Mmoja wa mashahidi ambaye aliheshimiwa sana na mahakama alikuwa ni Sheikh ambaye yeye alikiri ya kwamba aliwaona kwa uso wahusika wakuu. Huku ameshika Kurani Tukufu aliiambia Mahakama kwamba alimuona Muzaffar Ahmad na kijana mwingine wa Kiahmadiyya ambaye alikuwa pale Mahakamani kwamba wao ndio waliohusika katika kushambulia Msikiti wao. Muzaffar Ahmad

Endelea uk. 10

Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya yaweka Historia mpya

Na Swaleh Kitabu Pazi, MBBS. Dar es Salaam.

Kutoka toleo lililopita

Aidha alitumia pia fursa hiyo adhimu kuwapa khuddamul taarifa ya jengo la ofisi za tanzim linalojengwa na kuwajulisha maendeleo yake na sasa limefikia hatua ya kumalizia ujenzi huo katika hatua za mwisho kwa matumizi. Pia aliwafahamisha kuwa kwa sasa jengo hilo linatumiwa na Shule ya Sekondari Ahmadiyya kitonga kwa ajili ya ofisi na bweni kwa wanafunzi wa kiume na kuwaambia kuwa hizo ndizo fadhila za jengo letu tunazozipata na pia ni jukumu letu kama khuddam kuisaidia Jamaat kwa jambo lolote lililo ndani ya uwezo wetu kwani hiyo pia ni shule ya Jamaat na sisi ni uti wa mgongo wa Jamaat. Alisema.

Pia Sadr aliwakumbusha khuddam na Atfal wote kuelewa jukumu letu la kuchangia ujenzi wa jengo la ofisi zetu kwa hali mali na kwa kuwa sehemu kubwa ya ujenzi wa jengo hilo limechangiwa na khuddam wa Dar es Salaam sasa tuitumie fursa iliyopo kwa khuddam waliokuwa nje ya Dar es Salaam kupata fadhila hizo pia.

Pia Sadr alitumia muda huo kwa kuzungumza na khuddam na kuwakumbusha viongozi wenye dhamana ya kuongoza tanzim kutekeleza wajibu wao ipasavyo ikiwa ni pamoja na kuleta taarifa kwa wakati. Aidha Sadr aliwaomba waalimu wa matawi mbalimbali aliyopita kutusaidia kuunda safu za uongozi na alikumbusha kuwa tofauti na uchaguzi wa

Endelea uk. 11



Picha ya pamoja kati ya Wanajamaat wa tawi la Songea Mjini na uongozi wa Khuddamul Ahmadiyya taifa wakati ulipotembelea tawini hapo.